SportPesa
TZS. 595,659,980
NI YA KWAKO WIKI HII,
BETI LEO UWE MILIONEA
SPORTPESA.CO.TZ PIGA *150*87#



**LHRC** yashauri serikali kufikiria upya kujitoa mkataba haki Afrika

UKURASA 3




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Oktoba 23, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580742
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# Mswaki balaa jipya kuenea kwa corona



**DAWA** ya meno nayo yahusishwa iwapo...*Endelea ukurasa 2*



Rais wa Samia Suluhu Hassan, akimtambulisha mgeni wake, Rais wa Jamhuri ya Burundi, Évariste Ndayishimiye kwa viongozi mbalimbali wa Serikali, baada ya kuwasili katika viwanja vya Ikulu Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Tanzania, Burundi kushirikiana biashara, ulinzi na uchukuzi

UKURASA 2

UKURASA WA 3

### KESI YA SABAYA YAAHIRISHWA KISA SHAHIDI MGONJWA

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake sita, imeahirishwa katika Mahakama ya Hakimu...

UKURASA WA 4

### VIGOGO NIDA, MWANASHERIA IPTL WAFUTIWA MASHTAKA UTAKATISHAJI

VIGOGO watatu kati ya wanne wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Dickson Maimu, wamefutiwa mashtaka 10 ya...

## Kamera usalama kufungwa katika miji

UKURASA 3

**MICHEZO** AZAM, BIASHARA UNITED MAJARIBUNI UGENINI CAF UK.20

**MAONI, KATUNI** UK.6



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akionyesha nakala za mwongozo wa usajili wa wataalamu wa TEHAMA baada ya kuuzindua, katika Mkutano wa Tano wa Mwaka wa TEHAMA Tanzania, jijini Arusha, jana. Kushoto ni Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Ashatu Kijaji. **PICHA: OWM**

# Mswaki balaa jipya kuenea kwa corona

**Na Jaliwason Jasson,** SIMANJIRO

WATAALAMU wa afya wamebaini baadhi ya watu waliopona UVIKO-19 wanaugua tena ugonjwa huo ndani ya muda mfupi kutokana na kurudia mswaki baada ya kupona.

Kwa mujibu wa Ofisa Ufuatiliaji na Udhibiti wa Magonjwa wa Wizara ya Afya, Dk. Baraka Nzobo, ili kuepuka kuugua tena ugonjwa huo, mgonjwa anatakiwa kuteketeza kwa moto mswaki aliokuwa anautumia.

Dk. Nzobo alikuwa akitoa elimu jana namna ya kukabiliana na maambukizi ya UVIKO-19 kwa wananchi wa Mji Mdogo wa Mirerani wilayani Simanjiro mkoani Manyara.

"Mgonjwa aliyepona UVIKO-19, hapaswi kuutumia tena mswaki aliokuwa nao kabla ya kupona, kwa sababu atajiambukiza tena ugonjwa huo kupitia vijidudu vilivyobaki.

"Mswaki uliokuwa unautumia awali na kupata maradhi ya Uviko-19 na baadaye ukapata tiba ukapona, unatakiwa kuuacha kwa kuuteketeza na kutumia mswaki mpya ili usijiambukize upya ugonjwa huo," alifafanua.

Dk. Nzobo pia alisema ni hatari kuchangia dawa moja ya meno kwa familia nzima kupitia miswaki tofauti au watu wengi kutumia dawa moja ya meno hasa kwenye kambi za wazee na shuleni.

"Mnaposhirikiana dawa ya meno kwa kupigia mswaki na kusafisha kinywa kwenye hosteli, vyuoni au mikusanyiko yoyote ni hatari kwani huchangia kueneza maambukizi ya virusi vya UVIKO-19," alihadharisha.

Vilevile, Dk. Nzobo alisema watu wanatakiwa kuepuka kuchangia mswaki au kuhifadhi mswaki sehemu moja ili wajikinge na maambukizi ya Uviko-19.

Baadhi ya wakazi wa Mirerani akiwamo, Ally Suleiman, walisema elimu hiyo ya matumizi ya mswaki na dawa za meno kwenye mapambano ya Uviko-19, wengi wao ndiyo wameisikia kwa mara ya kwanza na wataitumia kuchukua tahadhari.

"Mimi nilikuwa nimezoea kuchukua tahadhari kwa kuvaa barakoa, kuepuka mikusanyiko, kunawa maji tiritika na kutumia vitakasa mikono, suala la kuchangia dawa ya meno kwenye mswaki kumbe ni tatizo, nilikuwa sijabaini hilo," alisema.

Aliwaomba wataalamu wa afya waendelee kutoa elimu ya janga la Uviko-19 kwani hivi sasa jamii ina mwamko mkubwa wa kuwasikiliza wao ndiyo maana wanashiriki chanjo.

Kwa mujibu wa Wizara ya Afya, hadi kufikia Oktoba 2 mwaka huu, Watanzania waliothibitika kuwa na maambukizi ya UVIKO-19 ni 26,034, vifo vilivyotokea ni 724 na waliopatiwa chanjo ni 885,579.

**KUHUSU CORONA**

Virusi vipya vya corona vinavyosababisha ugonjwa wa Uviko-19, viligunduliwa Novemba 2019 huko Wuhan, China na kwa Bara la Afrika mgonjwa wa kwanza raia wa kigeni aligundulika Misri.

Machi 16, mwaka jana, Tanzania ilithibitisha mgonjwa wa kwanza wa corona jijini Arusha ambaye aliwasili kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) akitokea Ubelgiji.

Msafiri huyo raia wa Tanzania aliondoka nchini Machi 3 mwaka jana na kati ya Machi 5 na 13, alitembelea nchi za Sweden na Denmark na kurudi tena Ubelgiji.

Siku iliyofuata, yaani Machi 17 mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alitangaza kufunga shule zote za awali, msingi na sekondari hadi kidato cha sita na baadaye vyuo vikuu kwa muda wa siku 30.

Kwa mujibu wa WHO, idadi ya wagonjwa wa corona duniani hadi wiki iliyopita, ni watu milioni 2.58 (takwimu halisi 2,258,909) na vifo vilifikia watu 154,388 huku Marekani, Italia, Hispania na Uingereza zikitajwa kuongoza kwa idadi ya wagonjwa na vifo.

# Tanzania, Burundi kushirikiana biashara, ulinzi na uchukuzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan na Rais wa Jamhuri ya Burundi, Evariste Ndayishimiye, wamekubaliana kuendeleza ushirikiano katika mambo mbalimbali ikiwamo mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Rais Samia alibainisha hayo jana alipozungumza na waandishi wa habari mara baada ya kumkaribisha Rais Ndayishimiye katika Ikulu ya Chamwino.

Alisema pamoja na mapambano dhidi ya UVIKO-19 pia wamekubaliana kuendeleza ushirikiano wa kibiashara ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa kutoka Umviza mkoani Kigoma hadi Burundi.

"Katika biashara tulikuwa tunashirikiana kutoka siku nyingi lakini kutokana na janga la UVIKO-19 biashara imeshuka sana lakini hii leo (jana) tumekubaliana kuwa tuendeleze ushirikiano ili kukuza biashara zetu," alisema.

Rais Samia alisema jambo lingine walilokubaliana ni kuimarisha ushirikiano kiusalama kwa kudumisha ulinzi katika mipaka baina ya nchi hizo.

Rais Ndaishimiye aliwasili jana jijini Dodoma majira ya saa nne asubuhi na kupokewa na Mwenyeji wake, Rais Samia.

Akizungumza na vyombo vya habari Ikulu ya Chamwino, Rais wa Burundi aliishukuru Tanzania kwa ukarimu wake na kuomba ardhi kwa ajili ya kilimo cha miwa.

"Tanzania ni ndugu zetu, sio marafiki, tunashukuru kwa kutukarimu kuanzia miaka ya 60, lakini tunaomba mtusaidie ardhi ya kulima kilimo cha miwa," alisema.

Rais wa Burundi alisema anaiomba Tanzania iwasaidie ardhi iliyopo katika mikoa inayopakana na Burundi ili iwe rahisi kwao kufanya kilimo hicho.

Rais huyo alisema katika kiwanda cha mbolea ambacho wamewekeza katika Jiji la Dodoma, wanatarajia kuajiri wafanyakazi zaidi ya 3,000 kutoka Burundi na Tanzania.

Pia aliishukuru Serikali ya Tanzania kwa kuwapokea Warundi tangu miaka ya 1960, akikumbusha namna Rais Jakaya Kikwete alivyowapa uraia wakimbizi zaidi ya 200,000 kutoka nchi hiyo.

"Kwa kweli Tanzania ilisimama kidete kuhakikisha amani inapatikana mpaka sasa Burundi imekua kiuchumi, kisiasa na wananchi wanaendelea kurudi nyumbani kwa kasi kubwa," Rais Ndayishimiye alisifu.

Rais huyo alitoa pongezi kwa Tanzania kuendelea kudumisha Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na kuendelea na uhusiano mzuri na Burundi katika nyanja za ulinzi na usalama.

# LHRC: Serikali itafakari kujitoa mkataba wa haki

**Na Waandishi Wetu**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) kimetoa wito kwa serikali kupitia upya uamuzi wake wa mwaka 2019 wa kujitoa katika mkataba wa nyongeza wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.

Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga, alitoa rai hiyo jana mkoani Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maadhimisho ya siku ya haki za binadamu Afrika.

Anna alisema serikali inapaswa kupitia upya uamuzi wake ili kuruhusu watu na taasisi kufungua kesi katika Mahakama ya Afrika.

"Leo (jana) ni siku muhimu kwa wapenda haki wote nchi za Afrika kwa kuwa Afrika inasherehekea kuanzishwa kwa mkataba wa Afrika wa haki za binadamu na watu wa mwaka 1981," alisema.

Kiongozi huyo alikumbusha kuwa mwaka 2019, serikali ilifanya uamuzi wa kujitoa katika ibara ya 34(6) ya mkataba huo ambao ilikuwa inaruhusu mtu au taasisi yoyote kuifikia Mahakama ya Afrika pale ambako kuna uhitaji wa kudai haki.

Alisema Tanzania imekuwa nchi ya pili baada ya Rwanda kujitoa katika mkataba huo unaoruhusu mtu au taasisi kufungua kesi dhidi ya serikali pale ambako kuna malalamiko ya kuvunja haki. "Ni wazi kwamba, watu pamoja na taasisi walitumia vizuri uwapo wa mkataba huu kwa kufungua kesi mbalimbali dhidi ya serikali kwa kuhitaji mabadiliko ya sheria, sera na mienendo kwa nchi.

"Kumekuwa na dhana na tafsiri isiyo sahihi kwamba, watu waliofungua kesi katika Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu, hawana nia nzuri na serikali kwa lengo la kuichafua. "LHRC inapenda kusahihisha dhana na tafsiri hiyo kuwa ni ishara ya kuimarika kwa demokrasia, ufikiaji wa haki, uvumilivu na uongozi bora," alisema.

Anna alisema LHRC inaamini kwamba muundo wa mahakama hiyo iliyopo Arusha ni wenye watu wenye kujua misingi ya kiafrika, tamaduni, taratibu za sheria na mazingira, hivyo kwa vyovyote uamuzi unaotolewa mahakamani humo ni wa haki na usawa.

Pia aliishauri serikali kuendeleza utamaduni wa kuripoti hali ya haki za binadamu kwa Umoja wa Afrika kupitia Mfumo wa Mapitio ya Haki za Bnadamu Afrika (APRM).

Alisema mara ya mwisho mapitio yalitolewa mwaka 2013 ambapo utekelezaji wake ulianza rasmi mwaka 2014.

"LHRC inatoa wito kwa taasisi za serikali hususani Jeshi la Polisi na vyombo vya usalama na wananchi kuzingatia haki za binadamu kwa kukuza na kulinda haki za binadamu katika kila ngazi," alisema.




Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari, mkoani Dar es Salaam jana, kuhusu maadhimisho ya Siku ya Haki za Binadamu Afrika. Kulia ni Ofisa Uchechemuzi wa kituo hicho, Raymond Kanegene. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kamera za usalama kufungwa katika miji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI Mkuu, Kassimu Majaliwa, ameiagiza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kufunga kamera za ulinzi kwenye maeneo muhimu ya mkakati ikiwamo miji na majiji ili kudhibiti matukio ya uhalifu.

Amesema kwa mujibu wa ripoti ya tathimini wa usalama duniani ya mwaka 2020 iliyoratibiwa na Shirika la Mawasiliano Duniani (ITU), Tanzania imeshika nafasi ya pili kwa Afrika katika ubora na ukomavu wa usalama wa mtandaoni.

Akizungumza jana jijini Arusha wakati akifungua mkutano wa tano wa TEHAMA wa mwaka, Waziri Mkuu aliipongeza Zanzibar kwa kuanza kufunga kamera ili kidhibiti uhalifu wa maeneo mbalimbali na kusisitiza wizara hizo kukaa pamoja na kuainisha jiji moja la mfano kati ya miji na majiji kuanza kufunga kamera hizo.

"Hii inatokana na jitihada zinazotekelezwa na serikali kupitia wizara hii iliyoundwa mahsusi kusimamaia sera ya TEHAMA, nitoe wito kuweka jitihada zaidi ili tathimini itakayofuata Tanzania iwe kinara barani Afrika," aliagiza.

Majaliwa alisema ili kufikia mpango huo, wizara ijikite kuimarisha kituo cha utafiti, ubunifu na uendelezaji wa TEHAMA ikiwamo kujenga uwezo na kuongeza matumizi ya teknolojia mpya ya kidijitali.

Alisema hiyo itasaidia kuendeleza serikali mtandao inayozingatia usalama wa mfumo wa taarifa za serikali na kurahisishia watumishi wa umma kiutendaji.

Kuhusu sensa ya watu na makazi, Majaliwa alisema wataalamu wa TEHAMA wahakikishe elimu sahihi kuhusu sensa inawafikia wananchi na zoezi zima la sensa ya mwakani linakamilika kwa ufanisi na viwango vya juu.

Waziri Mkuu pia aliagiza Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari kuwasilisha ofisini kwake kila mwaka kupitia Kituo cha uwekezaji Tanzania (TIC) mapendekezo ya vivutio vya uwekezaji katika sekta ya TEHAMA.

Aliiagiza Tume ya TEHAMA kuweka mikakati mahususi wa kusajili wataalamu wa TEHAMA ili kufikia lengo la usajili kutoka 700 hadi kufikia 5,000 mwaka 2025.

"Wizara ishirikiane na sekta binafsi katika kuongeza ufanisi kiutendaji kwa kufanya kazi na kampuni kubwa zilizobobea katika sekta hii ili kujenga uchumi wa kidijitali," aliagiza.

Kwa mujibu wa Majaliwa, serikali imetenga Sh. bilioni 170 kwa ajili ya kujenga Km 4,244 za Mkongo wa Taifa ili kufikisha Km 12,563 za Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano.

# Kesi ya Sabaya yaahirishwa kisa shahidi mgonjwa

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

KESI ya uhujumu uchumi inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, na wenzake sita, imeahirishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha, baada ya Jamhuri kuiomba mahakama kufanya hivyo kutokana na shahidi wa saba kuugua ghafla.

Katika kesi hiyo washtakiwa wengine ni Sylvester Nyegu (26), Enock Togolani (41), Watson Mwahomange (27), Jackson Macha (29) na Nathan Msuya (31) wanaokabiliwa na mashtaka matano ya uhujumu uchumi.

Akiomba ahirisho hilo jana mbele ya Hakimu Mkazi Patricia Kisinda katika mahakama hiyo, Wakili wa Serikali, Felix Kwetukia, aliomba mahakama iwape ahirisho la kesi hiyo hadi wiki ijayo kutokana na shahidi Ramadhani Juma ambaye ni mfanyakazi Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuugua ghafla.

"Mheshimiwa Hakimu kesi hii imekuja kwa ajili ya kusikilizwa na wiki hii tuliandaa mashahidi wanne, kati yao watatu tayari, sasa huyu shahidi wa wanne ameugua ghafla na hadi asubuhi hii, tumewasiliiana naye bado hayuko vizuri. Tunaomba ahirisho la kesi hii hadi wiki ijayo," aliomba.

Alidai kuwa nia yao kesi hiyo iendeshwe haraka na imalizike kwa haraka, hivyo aliomba ipangwe mwanzoni mwa wiki ijayo ili iendelee kusikilizwa.

Baada ya kuwasilisha ombi hilo, Wakili wa Utetezi, Moses Mahuna, alipinga ombi hilo na kuiomba mahakama isikubali kwa madai kuwa Jamhuri wana mashahidi 20 ambao walishawasema mahakamani hapo, hivyo hawana sababu ya kuomba kuahirishwa.

"Mheshimiwa Hakimu, naomba ikikupendeza ulikatae ombi hili kwa sababu Jamhuri wana mashahidi 20 na walitueleza hapa na mpaka sasa wametoa watatu tu bado mashahidi 17, hivyo kuugua kwa huyu mmoja kusitukwamishe. Walete hao wengine tuendelee nao sababu akiendelea kuugua hata mwaka ina maana tutakaa kumsubiri wakati mteja wetu anaendelea kusota ndani," aliomba.

Hoja hiyo iliungwa na wakili mwenzake upande wa utetezi, Fridolin Gwemelo, ambaye aliiomba mahakama kutokubali ombi la kuahirisha kesi hiyo kwa sababu upande wa Jamhuri unamashahidi wengi, hivyo walete wengine kesi iendelee.

Pia Wakili mwenzao upande wa utetezi, Edmund Ngemela aliunga mkono hoja za wenzake na kuiomba mahakama kutokubali ombi hilo na kudai kuwa haki inayocheleweshwa ni hasara kwa pande zote mbili.

Baada ya hoja hizo za kupinga ahirisho, Hakimu Kisinda alitoa nafasi kwa Wakili wa Serikali Kwetukia, ambaye aliomba mahakama hiyo kwa unyeyekevu kuahirisha kesi hiyo hadi wiki ijayo kwa sababu kuleta mashahidi wengine kwa jana ingekuwa vigumu kwa madai kuwa kuna hatua za kuwaleta mahakamani.

Alidai kuwa kila mmoja anafahamu hatua za kuomba shahidi aje mahakamani, hivyo haiwezekani kumpa wito wa kuitwa mahakamani shahidi ghalfa akaja na ni ngumu kwa kuwa hawakuwaandaa, hivyo ni vyema wakapewa nafasi hadi wiki ijayo.

Hakimu Kisinda alitoa uamuzi mdogo na kukubaliana na hoja ya Jamuhuri ya kuahirisha kesi hiyo na kuahirisha kesi hado Oktoba 27.

## Bil. 7/- kuboresha makazi ya wazee

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WIZARA ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, imetenga Sh. bilioni 7.4 kwa mwaka wa fedha 2021/22 kuboresha makazi ya wazee nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema hayo jana wakati akiwasilisha taarifa ya makazi ya wazee mbele ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii.

Dk. Gwajima alisema lengo la bajeti hiyo ni kuendeleza mpango wa wizara katika kukabiliana na tatizo la uchakavu wa miundombinu kwenye makazi hayo na kuweka mazingira mazuri kwa wazee wanaoishi katika maeneo hayo.

"Moja ya vigezo kwa mujibu wa mwongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa makazi ya wazee ni kuwa na mazingira wezeshi kwa wazee wasiojiweza pamoja na vifaa vya kumudu kupata huduma ndani na nje ya makazi, hivyo wizara imejipanga kuhakikisha makazi yote 14 yanayosimamiwa na serikali yanakidhi vigezo hivyo, vikiwamo majengo, umeme, maji safi na mifumo ya majitaka," alisema.

Gwajima aliongeza kuwa wazee 2,135 wamepata matunzo katika makazi ya wazee katika kipindi cha mwaka 2015 - 2020 na serikali inasimamia na kuratibu utoaji wa huduma kwa wazee katika makazi 20 yanayoendeshwa na taasisi binafsi pamoja na mashirika ya dini yenye jumla ya wazee 537.

Pia Dk. Gwajima aliwahimiza wananchi au taasisi zinazolenga kuanzisha makazi ya wazee kuzingatia taratibu wakati wa kuanzisha makazi hayo kwa kushirikisha mamlaka za maeneo husika ili kuhakikisha vigezo vyote vinazingatiwa.

Aliyataja mafanikio ya wizara katika kuendesha makazi hayo ni pamoja na uboreshaji wa miundombinu zikiwamo nyumba na miundombinu mingine ambapo makazi yaliofanyiwa ukarabati huo ni Nunge (Dar es Salaam), Kolandoto (Shinyanga), Njoro (Kilimanjaro), Magugu (Manyara), Kiilima (Kagera), Fungafunga (Morogoro) na Sukamahela (Singida).

"Huduma za chakula na mahitaji ya msingi zimeboreshwa pamoja na kuanzisha miradi ya bustani na ufugaji ambayo hutekelezwa na kusimamiwa na wazee wenyewe," aliongeza.

Naye Kamishna Msaidizi wa Ustawi wa Jamii, Mwanaisha Moyo, alisema wizara kupitia idara hiyo imejipanga kuhakikisha inawahudumia wazee walioko katika makazi ya wazee yanayosimamiwa na serikali ili kuhakikisha wanaishi vizuri na kupata mahitaji yote muhimu.

## Vigogo NIDA, mwanasheria IPTL wafutiwa mashtaka utakatishaji

**Na Hellen Mwango**

VIGOGO watatu kati ya wanne wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), akiwamo aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu, Dickson Maimu, wamefutiwa mashtaka 10 ya kutakatisha fedha katika kesi ya uhujumu uchumi.

Sambamba na vigogo hao, pia mwanasheria wa kampuni ya kufua umeme ya Independent Power Tanzania Limited, Joseph Makandage, naye amefutiwa shtaka la kutakatisha fedha katika kesi inayomkabili.

Kesi ya kina Maimu ilipangwa jana kwa ajili ya kutajwa mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Mbali na Maimu, washtakiwa wengine waliofutiwa mashtaka ni mshtakiwa wa tatu aliyekuwa Ofisa Usafirishaji, George Ntalima na mshtakiwa wa nne Xavery Silverius, maarufu Silverius Kayombo.

Awali, washtakiwa hao walikuwa wakikabiliwa na mashitaka 55, likiwamo la utakatishaji fedha na kuisababishia serikali hasara ya Sh. bilioni 1.175.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladslaus Komanya, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa, lakini Jamhuri inaomba kubadilisha hati ya mashtaka dhidi ya washtakiwa.

Alidai kuwa kesi hiyo iko kwenye hatua ya kusikilizwa ushahidi lakini Mkurugenzi wa Mashitaka (DPP), amekusudia kufanya marekebisho madogo chini ya kifungu cha 234(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA).

Wakili Komanya alidai kuwa hakutakuwa na pingamizi, wangeomba kuwasilisha hati mpya, lakini Hakimu Shaidi akasema hata wakiwasilisha hati , kesi hiyo haiko mbele yake na kutakiwa kuwasilisha mbele ya hakimu husika tarehe itakayopangwa.

Baada ya maelezo hayo, kesi hiyo iliahirishwa hadi Novemba 4, mwaka huu, itakapotajwa ambapo upande wa mashtaka utawasilisha hati mpya. Washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni aliyekuwa Meneja Biashara wa NIDA, Aveln Momburi na Mkurugenzi wa Sheria, Sajina Raymond.

Katika hatua nyingine, DPP amemwondolea mashtaka ya kutakatisha fedha aliyekuwa mwanasheria wa IPTL, Joseph Makandege.

Hatua hiyo ilifikiwa jana baada Jamhuri kuomba kubadilisha hati ya mashtaka dhidi ya mshtakiwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Ladislaus Komanya, alidai kuwa kesi hiyo ilipangwa kwa ajili ya kutajwa. Hata hivyo, alidai kuwa bado hawajafikia mwafaka katika majadiliano ya kukiri mashtaka kati ya mshtakiwa na DPP.

Katika hati mpya ya mashitaka, mshtakiwa huyo anakabiliwa na mashitaka matatu likiwamo la kuisababishia hasara serikali ya dola za Marekani 980,000.

Ilidaiwa kwamba shitaka la kwanza ni la kuongoza genge la uhalifu kuwa kati ya Oktoba 18, 2011 na Machi, 9 2014 ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, mshtakiwa ambaye si mtumishi wa umma, akishirikiana na watumishi wa umma, walitekeleza njama za hila ili kujipatia fedha .

Katika shitaka la pili ilidaiwa kati ya Januari 23 na Februari 10, 2014 katika benki ya Stanbic tawi la Kati, Wilaya ya Kinondoni na Benki ya UBL, Ilala, Dar es Salaam, kwa nia ya udanganyifu, alijipatia kutoka Benki Kuu ya Tanzania (BoT), Dola za Marekani 380,000 na Dola 600,000.

Shitaka la tatu ni la kuisababishia serikali ya Tanzania hasara kwamba, katika tarehe hizo, mshtakiwa aliisababishia serikali hasara ya jumla ya Dola 980,000.

Baada ya kusomewa mashitaka hayo, Hakimu alimtaka mshtakiwa huyo kutojibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina Mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo ya uhujumu uchumi.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Novemba 4, mwaka huu, kwa ajili ya kutajwa. Mshtakiwa amerejeshwa mahabusu.




Wananchi wakipita kwa shida kutokana na jenereta kubwa lililowekwa katikati ya njia ya waenda kwa miguu katika Mtaa wa Livingstone na Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## RC aonya biashara viungo vya binadamu

**Thobias Mwanakatwe,** MBOZI

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, amewaonya wakazi wa Mji wa Mlowo, wilayani Mbozi ambao wanajihusisha na biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu na uuzaji viungo vya binadamu. Kutokana na kuwapo kwa biashara hiyo, Mgumba ameonya kwamba watakaobainika watachukuliwa hatua kali za kisheria.

Amesema kwa sasa mji wa Mlowo unatajwa kuwa kitovu cha uratibu wa vitendo viovu, ikiwamo biashara ya kusafirisha wahamiaji haramu, uuzaji wa viungo vya binadamu na matukio ya ujambazi.

Alitoa tahadhari hiyo juzi wakati akiwahutubia wananchi, kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika eneo la kituo cha mabasi Mlowo, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya siku nne wialayani hapa kwa lengo la kukagua shughuli za maendeleo. Mkuu wa mkoa alisema serikali ina taarifa kuwa baadhi ya nyumba za kulala wageni katika mji wa Mlowo zimefadhiliwa na madalali na mawakala wa kusafirisha wahamiaji haramu kutoka Ethiopia na Somalia, ambao huitumia Tanzania kama njia ya kupita na kwenda katika nchi za kusini mwa Afrika, kwa ajili ya kutafuta maisha bora.

"Mlowo ambako mkuu wa mkoa anakaa imekuwa kitovu cha uratibu wa vitendo viovu likiwamo hili la kusafirisha na kuhifadhi wahamiaji haramu. Leo Tunduma wako nyuma, Ileje wako nyuma, Kyela wako nyuma. Shughuli yote iko hapa Mlowo," alisema. Nyumba za kulala wageni zinadaiwa kutumika kuwaficha wahamiaji haramu tunazijua, hivyo leo nimekuja kuwatahadharisha maana siku tukija kusimamisha biashara msilalamike kuwa tunaharibu mazingira ya biashara" alionya Mgumba.

Aidha, Mgumba alitumia hadhara hiyo kuwaonya watu wenye imani potofu wanaomini kuwa unaweza kutumia viungo vya binadamu kupata utajiri.

"Lakini suala la pili ninalotaka kuwaambia hapa ni hili la watu kudanganya kuwa unaweza kupata utajiri kwa kupeleka kiungo cha binadamu mwenzako kwa mganga wa kienyeji. Hili halikubaliki hata kidogo na wenye tabia hizo waache mara moja,' alisema.

Mgumba alisema inafika wakati kuna watu wanakubali kukodishwa, kwa ajili ya kutoa roho ya binadamu mwenzao ili kupata viungo na kuvipeleka kwa waganga wa kienyeji, ili kupata utajiri.

"Najua haya hayafurahishi masikioni mwenu, lakini lazima niwaambie. Hapa ndipo tunawakaribisha na kupokea watu waovu. Serikali iko macho tutamnasa mmoja mmoja na tutampatia haki yake kwa mujibu wa sheria maana serikali hii si ya makelele.

"Sisi tutatimiza wajibu wetu wa kisheria kuwalinda wananchi na mali zao na hakuna jambo litafanyika hapa Mlowo serikali isilijue au mimi mkuu wa mkoa kama mwenyekiti wa kamati ya ulinzi na usalama nisilijue," alisisitiza.

Mkuu huyo wa mkoa aliwataka wananchi kutoa ushirikianao kwa kuwa serikali ya mkoa imedhamiria kukomesha vitendo hivyo, ili kuweka mazingira ya mji huo na mkoa kuwa salama, kwa ajili ya shughuli za uchumi.

## AZAKI kujadili mpango maendeleo ya taifa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

ASASI za Kiraia (AZAKI) zinatarajia kuanza wiki yao leo jijini Dodoma huku miongoni mwa mambo yatakayofanyika ni majadiliano juu ya namna zinavyochangia kwenye utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa kwa miaka mitano.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kuhusu Wiki ya AZAKI, Mkurugenzi Mtendaji wa Asasi ya Umoja wa Mataifa (UNA-Tanzania), Reynald Maeda, alisema majadiliano hayo yatafanyika kwa siku tatu kuanzia Oktoba 25 hadi 28, mwaka huu.

"Kaulimbiu yetu ni mchango wa AZAKI katika maendeleo ya Tanzania na majadiliano yataongozwa na AZAKI zenyewe tukiangalia mchango wa AZAKI kwenye shughuli tunazofanya kazi mbalimbali zinaendaje kusaidia maendeleo ya nchi," alisema.

Maeda alisema wataangalia mchango wa asasi hizo kwenye utekelezaji wa Mpango huo ambao umezinduliwa Juni, mwaka huu.

"Tutaangalia na kuongezea mjadala uliofanyika hivi karibuni kwa hiyo tunaendelea kuangalia mchango wa AZAKI kwa taifa, na mazungumzo yatajikita hapo," alisema.

Pia alisema siku ya kilele, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, atatoa tuzo kwa baadhi ya AZAKI ambazo zimeonyesha mchango mkubwa kwenye maeneo zinayofanya kazi.

Naye Mkurugenzi Mkazi wa CBM Tanzania, Nesia Mahenge, alisema kabla ya majadiliano hayo, kutakuwa na maonyesho yatakayofanyika viwanja vya Jakaya Kikwete leo na kesho ambayo yatafunguliwa na Spika wa Bunge, Job Ndugai.

"Ufunguzi utatanguliwa na matembezi ya amani ya asasi za kiraia. Tunawahimiza wananchi kuhudhuria maonyesho haya na kupata ushauri wa kisheria, kujua kazi za AZAKI na mchango kwenye maendeleo ya taifa," alisema.

Alisema kutakuwa na zaidi ya washiriki 500 na kuhudhuriwa na wahisani wa maendeleo wakiwamo mabalozi kutoka nchi mbalimbali zikiwamo Denmark, Uswisi na Canada.

"Maendeleo yanayoletwa na AZAKI si ya kifedha tu bali katika maeneo mengine ikiwamo maendeleo ya wananchi kupitia miradi mbalimbali, kupinga ukatili wa kijinsia kwa wanawake na watoto na kuongeza ushirikishwaji wa wananchi kwenye ufuatiliaji wa rasilimali za umma," alisema.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato (TRA), Justine Katiti, akimwelimisha mfanyabiashara wa Wilaya ya Tunduru, mkoani Ruvuma wakati wa kampeni ya elimu kwa mlipakodi inayoendelea mkoani humo, juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Bunge lazibana taasisi za serikali kulipa madeni NHC

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imezibana wizara na taasisi za serikali kulipa malimbikizo ya madeni ya Sh. bilioni 26.75, ambayo zinadaiwa na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), ili litekeleze majukumu yake.

Akizungumza jana na waandishi wa habari baada ya kuwahoji viongozi wa shirika hilo kuhusu hoja za ukaguzi zilizoishia Juni 30, 2020, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Naghenjwa Kaboyoka, alisema pamoja na shirika kufanya kazi kwa weledi, kuna utitiri wa madeni ambao unasababisha kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

"Serikali tumeona inaipatia miradi mbalimbali NHC, ili iendelee kukua. Tumeona jitihada za bodi na mwenyekiti wake, menejimenti na watumishi wake. Kuna mategemeo hili shirika linatutoa kwenye kufa sasa tunaona linakua vizuri, tunaona kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa," alisema.

Aliagiza NHC kukusanya madeni hayo kwa watu binafsi na taasisi zinazodaiwa, ili kufikia malengo yake. Makamu Mwenyekiti wa PAC, Japhet Hasunga, alisema kamati imetoa maagizo sita, ikiwamo madeni hayo ya muda mrefu.

"Imeonekana kuna utiriri wa madeni na hayajakusanywa. Fedha ni nyingi sana kama zikikusanywa zitasaidia kutekeleza miradi ya shirika na kujitosheleza kimapato, tumeagiza madeni hayo yakusanywe." "Watu wengi wanadaiwa zikiwamo taasisi na wizara. Huu ni wakati mwafaka wa kuhakikisha taasisi zinalipa madeni, ili liwe na hali nzuri kifedha. Moja ya taasisi ni Wizara ya Afya inadaiwa Sh. milioni 692, hivyo tunaagiza ilipe, ili shirika lijitosheleze kimapato,"alisema.

Alizitaja taasisi zingine Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora (Sh. milioni 313), Wizara ya Fedha na Mipango (Sh. milioni 61.1), Wizara ya Kilimo (Sh. milioni 59.4), Bodi ya Korosho (Sh. milioni nne), Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo 9Sh. milioni 250.6), Baraza la Kiswahili (Sh. milioni 4.5), Shirika la Utangazaji Tanzania (Sh. milioni 33.6), Mkurugenzi wa Vijana Wizara ya Kazi (Sh. milioni 2.9) na Wizara ya Ardhi ambayo ni wizara mama ya shirika hilo Sh. Milioni 267.6. Hata hivyo, alisema kamati imeagiza kukamilisha kwa miradi yote ya nyuma ya shirika, ambapo kati ya miradi 26 iliyokuwa imesimama tayari 20 imekamilika.

"Tuliagiza huko nyuma wakamilishe miradi ambapo leo wamekuja wamesema imekamilika miradi 20 bado sita ipo kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji na wametueleza huko nyuma walikabiliwa na tatizo la fedha lilikwamisha kukamilika, lakini kwasasa serikali imeruhusu shirika kukopa, hivyo miradi itakamilika,"alisema.

Alitaja miradi hiyo sita ambayo ipo kwenye hatua mbalimbali ni mradi wa Morocco square, Plot 300, Kawe, Igunga, Makete na Iyumbu Nyumba 300.

Pia alitaka shirika litekeleze miradi iliyopewa na serikali kwa viwango vinavyotakiwa, ambapo kwasasa wamepewa jukumu la kujenga majengo ya awamu ya pili ya wizara saba kwenye Mji wa Serikali Mtumba, jijini Dodoma.

# Milioni 1.2 nchini wana matatizo ya macho

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

TANZANIA inakadiriwa kuwa na zaidi ya watu milioni 2.4 wenye matatizo ya kutokuona kwa viwango cha juu na kati.

Aidha, taarifa za Shirika la Afya la Dunia (WHO) zimeonyesha kuwa idadi kubwa ya watu wenye matatizo ya kutokuona, asilimia 89 wanaishi katika nchi za uchumi wa kati na wa chini, ikiwamo Tanzania.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi kwenye kilele cha maadhimisho ya Afya ya Macho Duniani na uzinduzi wa mwongozo wa kufundisha afya ya msingi na upokeaji taarifa duniani kuhusu uoni iliyofanyika kitaifa jijini hapa.

Dk. Gwajima alisema katika idadi hiyo, kuna watu milioni 1.8 wana matatizo ya kutokuona kwa kiwango cha kati na juu huku ikikadiriwa kuwa watu 640,000 wana matatizo ya kutokuona kabisa. Alibanisha kuwa visababishi vikubwa vya ulemavu wa kutokuona na upungufu wa kuona unazuilika kama vile upeo mdogo wa macho kuona na uoni hafifu vinarekebishika kwa kutumia miwani.

Alitaja viashiria vingine vinavyozuilika ni mtoto wa jicho na shinikizo la jicho na matatizo ya afya ya macho yanaathiri mtu wa umri wowote.

Pia alisema takwimu za hapa nchini zinaonyesha watu milioni 1.2 tu kwa mwaka 2020 ndio walifikiwa na huduma za macho katika vituo vya kutolea huduma za afya ikilinganishwa na uhitaji wa takribani watu milioni 12 na asilimia 38 tu ya watu wenye uhitaji wa miwani ya kurekebisha uoni ndio walipata tiba hiyo.

Kadhalika, alisema upasuaji wa mtoto wa jicho kwa mwaka jana, ulifanyika kwa wastani wa macho 200 tu kwa kila watu milioni moja ikilinganishwa na macho 2000 kwa kila idadi ya watu hao kama ilivyoshauriwa na WHO.

Aliongeza kuwa ugonjwa wa kisukari unaweza kuathiri macho yasipofanyiwa uchunguzi mapema na kuapatiwa matibabu kabla ya kupata athari kubwa na matumizi ya kopyuta na simu kwa muda mrefu yanachangia kuharibu afya macho . Mkurungenzi Mkazi wa shirika la Sightsavers, Godwin Kabalika, alisema matatizo ya macho bado yapo na wagonjwa wamekuwa wakiongezeka kila mwaka na takwimu za Dunia zinaonyesha takribani watu bilioni 2.2 wana upungufu wa kuona .

Kabalika, alisema kati ya hao watu bilioni moja wanatatizo ambalo yangezuilika kama lingeshughulikiwa mapema na idadi imekuwa ikiongezeka kutokana na ongezeko la idadi ya watu.

Pia alisema ili kukabiliana na ongezeko hilo inahitajika kuongezeka kwa kasi za afua za kukabiliana na tatizo hilo na afya ya macho iwe sehemu ya afya kwa wote pamoja na kuhamasisha tafiti zaidi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Twiga Stars peperusha vyema bendera ugenini

**KALENDA** ya mashindano ya kimataifa kwa upande wa ngazi ya nchi inaendelea leo ambapo Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake maarufu Twiga Stars inatarajia kushuka ugenini Afrika Kusini kurudiana na wapinzani wao, Namibia.

Timu hizo zinakutana katika kusaka nafasi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wanawake ambazo zitachezwa mwakani.

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam, wageni waliibuka na ushindi wa mabao 2-1.

Kwa matokeo hayo, Twiga Stars ambayo inafundishwa na Kocha Mkuu, Bakari Shime na hivi karibuni ilitwaa ubingwa wa mashindano ya COSAFA, bila kupoteza mchezo hata mmoja, inahitaji kupata ushindi mnono ili kusonga mbele katika michuano hiyo.

Hata hivyo leo timu hizo mbili zinakutana katika uwanja huru, baada ya Namibia kuuchagua Uwanja wa Soweto ulioko Afrika Kusini kutumika kama uwanja wake wa nyumbani.

Mechi hiyo inatarajiwa kuwa na ushindani kwa pande zote mbili, lakini Twiga Stars inaonekana itakuwa kwenye presha zaidi kwa sababu itahitaji kufuta makosa waliyofanya katika mechi yao ya awali ambayo walicheza mbele ya mashabiki wao.

Katika mpira wa miguu lolote linaweza kutokea na kinachoweza kutoa majibu sahihi ni kusikia filimbo ya mwisho baada ya kumalizika kwa dakika 90.

Tunaamini Shime na benchi lake la ufundi limeshayafanyia kazi mapungufu yote na leo watashuka uwanjani wakiwa makini na wenye utulivu wa kuhitaji 'kupindua meza' na hatimaye kuendelea katika hatua inayofuata ya mashindano hayo yanayosimamiwa na kuandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Kama Namibia walicheza vyema na kupata ushindi wakiwa kwenye ardhi ya Tanzania, basi hilo linawezekana kwa Twiga Stars kupambana na hatimaye kuwaondoa wapinzani wenu kwenye michuano hiyo mikubwa inayoendelea hapa barani Afrika.

Soka ni suala la kujipanga vyema na kutumia vizuri nafasi ambazo mtazitengeneza, utulivu na umakini ndio silaha kuu ambayo inaweza kuwafanya Twiga Stars mkamaliza dakika 90 zilizobakia za ugenini mkiwa na shangwe ambayo inasubiriwa kwa hamu na mashabiki na wadau wa soka hapa Tanzania.

Mbali na Twiga Stars, Simba, Azam FC na Biashara United pia zinakabiliwa na majukumu ya kimataifa katika mechi za marudiano za Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho.

Klabu hizo zilipata matokeo mazuri katika mechi zao za kwanza, lakini tunawakumbusha kuwa bado hawajamaliza kazi mpaka watakaposikia filimbi ya mwisho imelia.

Kuna wakati mpira unakupa matokeo katili, ili matokeo hayo yasije kwa upande wa klabu za Tanzania, ni vyema wachezaji wakajipanga kujituma kusaka matokeo chanya na kumalizia kazi nzuri ambazo walizianza.

Kufanya vyema kwa timu hizo, zitaihakikishia Tanzania kupata uwakilishi wa klabu nne katika mashindano hayo ya kimataifa mwakani na kama zote zitashindwa kuingia makundi, basi tutajiweka kwenye nafasi ya sintofahamu.

Tayari Azam ilishafika Misri kwa ajili ya kurudiana na Pyramids wakati Simba itakayowakaribisha Jwaneng Galaxy kutoka Botswana yenyewe imeshakaa sawa na imara kuendelea pale ilipoishia, lakini Nipashe ikiwataka Biashara United kuongeza umakini watakapokuwa ugenini kurejeana na Al Ahly Tripoli.

Tunawakumbusha mpira ni ajira, hivyo wachezaji wa timu zote zinazokabiliwa na mashindano ya kimataifa wanatakiwa kucheza kwa viwango vya juu ili kujiweka sokoni au kumvutia Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Kim Poulsen kuwaita kwenye kikosi chake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Aali hupatikana kwa ghali

Na Barnabas Maro

**KITU** kizuri au bora huwa ghali au hakipatikani kwa urahisi. Hii ni methali ya kutumiwa kuwaonya watu kuwa sharti wawe tayari kuvumilia shida au matatizo kabla ya kufanikiwa wajue kuwa kitu kizuri hakipatikani hivi hivi tu.

Nchi ni eneo la ardhi lenye utawala wake; dola. Sehemu ya ardhi ambayo imegawanywa kwa mipaka ya kisiasa na inayotambulika kwa jina la taifa lake. Kwa mfano Tanzania, Kenya, Uganda, Afrika Kusini, China, India, Marekani, Ufaransa, Italia n.k. Wazawa wa nchi huitwa wananchi yaani raia wa nchi husika.

Kwa maana nyingine ni kama nasaba yaani uhusiano wa kizazi baina ya watoto na wazazi au wazee wao; = uzawa; utungo. Pia uhusiano wa watu wenye uzao mmoja, uhusiano wa watu wanaotokana na ukoo mmoja. Kwa hiyo ingawa Tanzania ni nchi yenye mikoa mingi kama zilizvyo nchi zingine duniani, twapaswa kufuata taratibu zilizowekwa na Serikali yetu ambayo ni chombo kikuu kabisa chenye mamlaka ya kuendesha utawala wa nchi, chenye wizara mbalimbali.

Udugu, pia undugu ni uhusiano wa watu wanaotokana na uzawa mmoja; =ujamaa. Ndo maana marehemu Rais Julius Kambarage Nyerere (Mungu amrehemu) alisema makabila yote 120 yaliyokuwapo wakati ule yazungumze lugha moja yaani Kiswahili ili tuelewane. Hakuishia hapo kwani alisema watu wote tuitane ndugu bila kubaguana na ikawa hivyo.

Kwa ajili hiyo watu hawaoani kikabila kama ilivyokuwa zamani. Hakuna kubaguana kwani sote ni ndugu. Lugha ya Kiswahili yazungumzwa na makabila yote nchini na huelewana hata kama si wote wanaozungumza kwa ufasaha.

Upendo ni hali ya kuvutia moyoni na mtu au kitu; huba, mapenzi. Hali ya mtu kuvutiwa na kimapenzi na kitu, mtu au jambo. Ni kweli kuwa Yanga na Simba zilikuwa moja mwaka 1935 kisha kutengana mwaka 1936 na sasa utadhani ni timu za nchi tofauti zenye uhasama usiozuilika.

"Ajabu" ni kitu kisicho cha kawaida, cha kushangaza na kustajabisha, -kigeni, si -a kawaida -a pekee, -a kioja. Inanilazimu kueleza yote haya kwani Simba na Yanga utadhani ni watu wa mataifa mawili waliohujumiana, kupigana na kuwekeana shonde yaani hali ya watu kutozungumza pamoja kutokana na kugombana.

Sivyo bwana. Hawa ni watu wa Taifa moja la Tanzania tena wa mkoa mmoja na jiji moja litwalo Dar es Salaam na kama haitoshi, makao ya vilabu vyao vipo maeneo ya Kariakoo. Kinachowafanya waingize tofauti zao mpaka kwenye timu za Taifa ni nini?

Ndio maana "Ukistaajabu ya Musa utayaona ya Firauni." Maana yake ukishangaa kutokana na miujiza ya Musa utashtuliwa na matendo ya Firauni. Matumizi yake ni sawa na: "Ukistaajabu ya chawa huona ya kunguni."

Ni ajabu na kweli kwamba wanaokwenda kuangalia mechi za Simba na Yanga uwanjani ni wengi maradufu (ongezeko la mara mbili la kitu cha awali) kuliko wanaokwenda kuziangalia timu zetu za Taifa zinapopambana na timu ngeni za mataifa ya nje!

Hapana shaka huwa tunachekwa na kudharauliwa sana na timu za mataifa mengine zinapokuja kupambana na timu zetu humu nchini! Twachekwa kwa ujinga wetu.

Timu zetu za Taifa zinapopambana na timu za mataifa mengine, ni watu wachache wanaokwenda uwanjani kushangilia, tofauti kabisa zinapopambana Simba na Yanga ambazo hujaza watu pomoni yaani jaa hadi juu, tele, sufu sufu. Katika hali ya kujaa au kuwa -ingi. Ni ajabu lakini ndio ukweli wenyewe!

Kumbe ndo maana wahenga walisema: "Akili ni mali." Kwamba akili ni sawa na mali. Haiwezekani mtu akafanya jambo likawa kama hana akili. Methali hii hutumiwa kumrejelea mtu ambaye anatenda mambo ya kufikiri au kutumia akili.

Pia husemwa: "Akili ya mtu ndio wazimu wake." Yaani akili ya mtu yaweza kuwa wazimu wake pia. Methali hii hutumiwa kuelezea kuwa akili ya binadamu inaweza kuzua mema na mabaya pia.

Bila shaka methali hii inayofuata itatoa usingizini kwamba: "Mtambua ndwele (ugonjwa) ndiye mganga." Maana yake anayegundua ugonjwa ndiye tabibu anayeweza kuirekebisha. Kwa maana hiyo tunapaswa kuzinduka ili tujirekebishe na kuondokana na ubozi (upumbavu) wetu.

Je, mwajua kuwa "urafiki ni mzuri lakini udugu huzika mtu?" Maana yake urafiki ni kitu kizuri lakini tunapaswa kuwathamini jamaa zetu kwa kuwa ndio wanaoweza kutufaa wakati wa shida au hata kutuzika tunapofariki.

# Maelfu kunufaika na miradi ya RUWASA

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAKRIBAN wananchi 94,186 wa halmashauri za Msalala na Kahama mkoani Shinyanga, wanatarajia kunufaika na miradi ya maji safi na salama inayotekelezwa na Wakala wa Usambazaji wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), yenye thamani ya Sh. bilioni 18.674.

Miradi hiyo inatekelezwa katika kata za Bulyanhuru-Kakola, Busangi, Bugarama-Ilogi Halmashauri ya Msalala na mtaa wa Nyashimbi kata ya Mhongolo katika Manispaa ya Kahama.

Meneja wa RUWASA Kahama, Maduhu Magili, aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya ujenzi wa miradi hiyo mbele ya kamati ya ulinzi na usalama ya wilaya iliyoongozwa na Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga.

Alisema kati ya miradi minne ya maji inayojengwa na RUWASA, miwili ya Nyashimbi na Kakola imeshakamilika na wananchi wanaendelea kunufaika na huduma ya maji kutoka Ziwa Victoria.

Awali, Kiswaga aliitaka RUWASA kuhakikisha wanakamilisha miradi mingine ya maji ili kuendelea kutoa huduma kwa wananchi na kuwaondolea shida hiyo.

"Mkuu wetu wa mkoa ameagiza fedha zote zilizotolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ajili ya wananchi hazitakiwi kukaa kwenye akaunti ndani ya siku saba hazijatumika nami naagiza fedha za miradi ya maji hazitakiwi kukaa ndani ya siku tatu hazijatumika na endapo zikikaa zaidi nitawawajibisha," alisema.

Kiswaga aliitaka RUWASA kutumia Sh. milioni 70 zilizotolewa kwa ajili ya ulazaji wa mabomba ya maji kutoka katika chanzo cha maji hadi tangi kuu na kazi hiyo ihakikishe inawapatia vijana.

Mmoja wa wanufaika wa miradi hiyo, Sebastian Chacha, mkazi wa kata ya Busagi alisema wanawake na watoto wa kike wamenusurika kuliwa na fisi nyakati za alfajiri wanapokwenda kata jirani ya Ngaya kutafuta maji.



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi Benki ya Biashara ya Walimu Tanzania, Francis Ramadhani (wa tano kushoto) na wajumbe wa bodi hiyo, wakisherehekea miaka mitano tangu kuanzishwa kwa benki hiyo, iliyokwenda sambamba na Mkutano Mkuu wa Tano wa Wanahisa, jijini Arusha jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC: Marufuku ubomoaji vibanda vya magazeti

**Na Richard Makore,** MWANZA

MKUU wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, ameagiza watendaji wanaosimamia na kuratibu uondoaji wa machinga mkoani hapa, kuacha kuviondoa vibanda vya kuuza magazeti kwa kuwa hiyo ni huduma na si biashara.

Akizungumza na waandishi wa habari jana ofisini kwake jijini hapa, Gabriel alisema hakuwa na taarifa kwamba vibanda hivyo vimeondolewa na kutaka uwapo utaratibu maalum wa kuviainisha vyote, ili vibaki vilipokuwa.

"Magazeti ni huduma na si biashara, hivyo lazima wahusika mkutane na uongozi wa mkoa, ili kuona namna bora ya kuainisha vibanda vyote vya kuuza magazeti, ili vibaki sehemu zake, "alisema.

Gabriel pia alisema kesho itakuwa siku ya usafi wa mazingira katika Jiji lote la Mwanza, ili kuliweka safi baada ya kuondolewa machinga.

Alisema barabara zote zinatakiwa kufanyiwa usafi, ili kuliweka jiji katika hali ya usafi na kwamba viongozi wote jijini hapa wasimamie mpango huo.

Mkuu huyo wa mkoa alisema Jiji la Mwanza linazalisha tani 1,120 za takataka kwa siku na kwamba asilimia 75, zinazolewa na kupelekwa kutupwa kwenye dampo.

Aliwaagiza wakurugenzi wa manispaa na halimashauri katika Mkoa wa Mwanza kuangalia vigenzo vya kampuni za kuzoa takataka zilizopo, ili kubaini ambazo hazifanyi kazi vizuri na kuziondoa.

Gabriel aliongeza kuwa suala la usafi kwa sasa litakuwa agenda ya kudumu, ili kuliweka safi jiji hilo na kwamba kila mmoja anao wajibu wa kuhusika na mpango huo.

Kuhusu taa za barabara kutowaka baadhi ya maeneo jijini Mwanza nyakati za usiku, Gabriel aliagiza mamlaka zinazohusika kurekebisha tatizo hilo kwa haraka.

Akizungumzia machinga kuhamia maeneo rasmi, Gabriel alisisitiza kwamba mpango huo ni endelevu, lakini hautatumia nguvu katika utekelezaji.

"Hatutatumia nguvu kabisa katika suala hili la kuondoa machinga, badala yake tutajikita katika kutoa elimu kwa machinga wote, ili waondoke kwa hiari kwenda maeneo rasmi waliyotengewa," alisema.

Wakati mkuu huyo wa mkoa akitoa kauli hiyo jana, watumishi wa jiji wakiwa na magari, juzi walipita katikati ya jiji na kuzoa vibanda vya machinga na kuondoka navyo pamoja na kuwakamata wamiliki wake.

# Wanufaika TASAF wapewa darasa fedha

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WANUFAIKA wa Mpango wa Uhawilishaji fedha kwenye kaya maskini unaotekelezwa na serikali kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), wilayani hapa, wamekumbushwa kuzitumia fedha hizo kwa malengo.

Wameshauriwa kuwa pindi mradi utakapokwisha wawe na kitu cha kuonyesha tofauti na sasa ambapo wananchi wengi wamekuwa wakinunua nyama, unga na mchele ili kula vizuri.

Maelekezo hayo yalitolewa jana na Mtendaji wa Kata ya Majengo, Mohammed Senjele, wakati akizungumza na wakazi wa vijiji vya Majengo na Muungano wanaonufaika na mpango huo wa TASAF.

Senjele alisema takwimu zinaonyesha kuwa Sh. 12,542,000 zimekuwa zikiingia kwanye mzunguko wa fedha katika kata yake kila inapotokea TASAF wanalipa fedha kwanufaika 354 waliotambuliwa na kuandikishwa katika mpango huo tangu kuasisiwa kwake na serikali mwaka 2013.

Hata hivyo, alisema kinachoshangaza ni kuona familia hizo zinaendelea kuishi katika mazingira magumu pindi wakisubiri malipo hayo. Alisema katika kijiji cha Majengo kuna wananufaika 166 ambao kila kinapofika kipindi cha malipo, serikali huwapelekea Sh. 5,718,000, Kalanje chenye wanufaika 116 huingiziwa Sh. 4,270,000 na Muungano chenye wanufaika 72 hupelekewa Sh. 2,554,000.

Mmoja wa wanufaika hao, mkazi wa kijiji cha Majengo, Fatuma Mtesa, alisema kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini kupitia TASAF, amefyatua matofali ambayo na kujengea banda la kufugia kuku wa kienyeji, bata na kuku wa kisasa ambao amekuwa akiwauza na kupata fedha ambazo humsaidia kununua mbolea na shughuli za shambani.

Naye Fatuma Gwasa alisema TASAF imemwezesha kujenga nyumba ya bati yenye vyumba vitatu na sasa anafuga kuku na bata na kwamba amenunua ng'ombe wa maziwa ana shamba ambalo limekuwa likimpatia mazao ya kutosha.

Alisema mazao hayo amekuwa akiyauza na mengine kula na kwamba hata ikifikia mpango unafika mwisho, hatatetereka. Alitumia nafasi hiyo kuishukuru serikali kupitia mpango huo kwa kuzijali familia zinazoishi katika kaya maskini uliopindukia.

Mratibu wa TASAF Wilaya ya Tunduru, Muhidini Shaibu, alisema awamu hii wanalipa Sh. 488,362,000 kwa wanaufaika kutoka katika kaya 12,740 zilizoko katika vijiji 88 vilivyosajiliwa kunufaika na mpango huo.

# Walipakodi waongezeka

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Geoffrey Mwambe, amesema kumeshuhudiwa ongezeko kubwa la walipakodi kwa hiari katika uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Amesema hali hiyo imechangiwa na mikakati mbalimbali ya serikali kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Waziri huyo amesema imeshazifungulia akaunti zote za wafanyabiashara na wadau wa sekta binafsi zilizokuwa zimefungiwa, ili kuruhusu kuendelea kufanya kazi na kuongeza mzunguko wa fedha.

Mwambe alibainisha hayo juzi jijini Dar es Salaam alipofungua mkutano wake na wadau wa sekta binafsi kujadili fursa za fedha za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Umekuwa ni msimamo wa Rais Samia kuwa serikali iache miradi inayoweza kufanywa na sekta binafsi ifanye kwa sababu ndio sekta inayoweza kutengeneza ajira nyingi nchini. "Mfano mzuri sasa akaunti zote za wafanyabiashara zipo 'free' (huru), makusanyo ya mwezi uliopita yalikuwa Sh. trilioni 1.8, watu wamelipa kodi kwa hiari na mapato yamekuwa yakipanda kwa asilimia 12 bila kutumia nguvu," alisema. Waziri huyo alisema serikali inaendelea kuboresha mazingira ya kuvutia wawekezaji na kushirikiana na sekta binafsi ili kuongeza mzunguko wa fedha kwa wananchi, kuongeza mapato na uchumi wa taifa.

Baadhi ya miradi ambayo serikali inashirikiana na sekta binafsi kuitekeleza ni ya shule na hospitali katika ununuzi wa vifaa na ukarabati wa majengo na muda wa miradi hiyo ni miezi tisa.

Mwenyekiti wa Benki zote nchini, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela, alisema serikali kushirikisha sekta binafsi katika miradi yake kutaisadia kuongeza mzunguko wa fedha nchini.

"Hii ni historia kama miradi yote ya nchi itakwenda hivi, kila mtu mtaani atakuwa na fedha, kodi zitaongezeka.

"Benki zipo tayari kushirikiana na sekta binafsi pia tupo tayari kutoa mikopo ya muda mfupi ili kusaidia utekelezaji wa miradi mbalimbali inayotolewa na serikali kwa sekta binafsi," alisema Nsekela. Alibainisha kuwa miradi hiyo ya thamani ya Sh. trilioni 1.3 kupitishiwa kwa wadau wa sekta binafsi ni kiasi kikubwa kitakachosaidia kuongeza mzunguko wa fedha nchini.

Mmoja ya wadau hao wa sekta binafsi, Dk. Albart Katagira, aliiomba serikali kuongeza malipo ya awali ya miradi wanayopewa na serikali kutoka asilimia 16 za sasa hadi asilimia 50.




Naibu Gavana wa Benki Kuu, Dk. Bernard Kibese (katikati), akiagana na Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya NMB, Dk. Edwin Mhede, baada ya uzinduzi wa Mfumo wa Majaribio ya Kiteknolojia (SADNDBOX), unaotoa fursa kwa wajasiriamali wa teknolojia kujaribu ugunduzi wao kupitia benki hiyo, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya NMB, Ruth Zaipuna. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LSF yapongezwa huduma za kisheria

**Na Frank Monyo**

MKURUGENZI wa Idara ya Msaada wa Kisheria kutoka Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Visiwani Zanzibar, Hanifa Ramadhan Said, amesema kupitia programu ya Shirika la Legal Services Facility (LSF) na wadau wake nchi nzima, kumewezesha kwa kiasi kikubwa kusaidia jamii kupitia uwezeshaji wa kisheria.

Amesema LSF pia imesaidia kuundwa na kupitisha kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017 iliyofanya kazi za watoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria kutambulika.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dodoma wakati akifungua mkutano wa siku mbili uliowakutanisha wadau wake kutoka Tanzania Bara na Zanzibar kufanya tathimini ya utekelezaji wa program ya upatikanaji haki kwa mwaka 2021.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Hanifa alisema mkutano huo ni muhimu kwa kuwa unawaleta pamoja wadau wa msaada wa kisheria ambao wamekuwa ni sehemu kubwa ya mafanikio katika kukuza upatikanaji wa haki nchini.

Alisema moja ya mafaniko ni kushirikiana na Jeshi la Polisi kulipa msaada wa zaidi ya Sh. milioni 400 ili wapitie mwongozo wa jeshi lao (PGOs) na hiyo kuwa fursa ya kurasimisha rasmi uwapo wa madawati wa wanawake na watoto katika vituo vya polisi.

"Mkutano huu ni muhimu sana kwa wadau wa sekta ya msaada wa kisheria. Kumekuwa na tabu mbalimbali katika jamii ambazo husababishwa na ukandamizaji wa haki mbalimbali ikiwamo wanawake na watoto.

"Kupitia programu ya LSF na wadau wake nchini mmeweza kufanya kazi kubwa ya kusaidia jamii kupitia uwezeshaji wa kisheria," alisifu.

Alisema kuwa mkutano huo ulijumuisha washiriki takribani 200 ikiwamo watendaji wakuu wa mashirika ya watoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria kutoka mikoa yote nchini.

Aliongeza kuwa mkutano huo unalenga kutoa wigo wa kubadilishana taarifa kuhusu matokeo ya programu na kujadili pamoja kwa umuhimu na kimkakati mafanikio ya LSF kwa miaka ijayo baada ya mwaka 2021 kwa wanufaika na wadau wote wa LSF.

"Hii inakuja kuelekea utekelezaji wa mpango mkakati mpya wa LSF wa miaka mitano ijayo unaotarajia kuanza mwakani mpaka 2026.

"Mkutano huu unalenga kukuza ufanisi wa kiutendaji, utoaji wa huduma, ushirikishaji wa wananchi katika mifumo ya huduma za msaada wa kisheria kwa ajili ya kuchochea ukuaji na ustawi wa uwajibikaji, ushiriki na ujumuishwaji wa raia katika mifumo ya uwezeshaji wa kisheria nchini," alisema.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa LSF, Lulu Ng'wanakilala, alisema amefurahi kukutana na wadau wake wote ambao amekuwa akifanya nao kazi nchi nzima, ambapo kwa kipindi cha miaka 10 wamepata mafanikio mbalimbali ikiwamo kuundwa kwa Sheria ya Msaada wa Kisheria ya Mwaka 2017.

"Ninafurahi kukutana na wadau wetu wakubwa ambao mmekuwa mkifanya kazi kubwa ya kutekeleza program yetu ya upatikanaji haki nchi nzima.

"Ninaona fahari kuona kuwa LSF sasa imetimiza miaka 10 tangu ianze kutekeleza programu yake na kupitia mashirika wanufaika wake tumefikia mfanikio mbalimbali ya sekta ya msaada wa kisheria.

"Ninaamini kuwa baada ya kikao hiki kazi yetu itaendelea kwa kasi zaidi ili kuwa na jamii iliyowezeshwa kisheria kupitia huduma bora za msaada wa kisheria," alisema Ng'wanakilala.

Wakili wa Serikali kutoka Wizara ya Katiba na Sheria, Agness Mkawe, alisema anaamini kuwa zoezi la tathmini ya utekelezaji wa programu ya upatikanji wa haki nchini litakwenda sambamba na wadau wote wa sekta ya msaada wa kisheria kuelekezana kuhusu kutii matakwa ya kisheria juu ya uendeshaji wa taasisi au mashirika yanatoa huduma za msaada wa kisheria na wasaidizi wa kisheria nchini.

## Benki yatoa bilioni 28/- kwa wafanyabiashara

**Na Mwandishi Wetu**

KUTOKANA na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19, Benki ya Afrika Tanzania imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 28 kwa wafanyabiashara wadogo na wa kati (SMEs), ili kuwawezesha kuendeleza na kukuza biashara zao.

Uongozi wa benki hiyo umesema mikopo hiyo imetolewa kwa kuzingatia ukweli kwamba asilimia 95 ya biashara zote nchini zinatoka katika sekta hiyo.

"Tumetoa mikopo kwa jumla ya wafanyabiashara 49 nchi nzima. Tukiweza kusaidia kutoa mikopo na kuwasaidia waweze kukua zaidi, tutakuwa tumechangia pia katika ukuaji wa uchumi wa nchi kwani watatoa ajira na biashara zao zitadumu," alisema Mkurugenzi wa Benki hiyo, Adam Mihayo, alipozungumza katika hafla ya utambulisho.

Hafla hiyo ilihudhuriwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika, Amine Bouabid, mabalozi na baadhi ya wateja.

Mihayo alisema maono ya benki hiyo yanaendana na maono ya serikali katika kukuza uchumi na kwamba uamuzi wa kuanzisha mkopo kwa wafanyabiashara kipindi cha mlipuko wa UVIKO-19 kinalenga kukuza biashara, kutengeneza ajira na kukuza uchumi.

"UVIKO-19 uliathiri uchumi wa dunia pamoja na Tanzania, lakini kwetu athari hazikuwa kubwa sana kwa sababu tuna sekta nyingi zinazochangia katika uchumi tofauti na nchi nyingine ambapo sekta moja inachangia zaidi kuliko zingine," alisema.

Aliongeza kuwa mikakati ya serikali katika kukabiliana na janga la UVIKO-19 pamoja na jitihada za Benki Kuu ya Tanzania (BoT) kuja na mikakati na sera za kuhakikisha kwamba uchumi hauathiriki, zimefanya Tanzania kuendelea kufanya vizuri kiuchumi kulinganisha na nchi nyingine za kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Afrika, Amine Bouabid, alisema amekuwa katika ziara Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania kuangalia utendaji kazi na pia kuweka mipango kwa ajili ya miaka miwili ijayo (2022-2024).

Bouabid aliongeza kuwa nchi inategemea kwa kiwango kikubwa wafanyabiashara wadogo katika kuleta maendeleo ya kiuchumi.

"Tutafanya kazi kwa ukaribu zaidi na sekta hii kwani biashara zao zikikua vizuri zinatengeneza ajira na kukuza uchumi.

"Benki yetu imekuwa ikitoka mikopo mingi kwa wafanyabiashara wa Afrika Mashariki ukilinganisha na nchi zingine upande wa magharibi mwa Afrika," alisema.



# Aagiza kuanzishwa kitengo kilimo hai

**Na Faustine Feliciane**, DODOMA

NAIBU Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, ameagiza wizara hiyo kuunda kitengo maalum kwa ajili ya kilimo hai pamoja na kuanzisha benki ya mbegu.

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa kongamano la pili la kitaifa la kilimo hai, Bashe alisema wizarani kuna dawati la kilimo hai lakini kwa sasa kuna haja ya kutengewa kitengo chake na kuwekewa bajeti yake.

Bashe alisema maisha ya usoni kilimo hai kitakuwa kimbilio la wananchi kuepuka magonjwa yanayotoka na vyakula.

"Lakini pia naiagiza Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) nao kuanzisha kitengo ambacho kutakuwa kukifanya utafiti juu ya kilimo hai hasa kwenye mbegu. Mimi nitakuwa mtetezi na msemaji wa kilimo hiki ndani ya wizara," alisema Bashe.

Pia alisema wakati umefika kwa taifa kuwa na benki yake ya mbegu za asili kwa ajili ya kuwasaidia wakulima nchini.

"Sasa hivi hata mbegu hizi tunazotumia za asili upatikanaji wake pia ni changamoto. Sasa tushirikiane na wadau na wizara iko tayari sasa kushirikiana kuanzisha benki ya mbegu zetu za asili. Naamini baada ya kongamano hili mtaleta mapendekezo yenu," alisema.

Alisema kwenye bajeti ya mwaka ujao wa fedha, wizara itatenge bajeti kwa ajili ya kilimo hai lengo likiwa kukiinua Kilimo hai.

Naye Waziri wa Kilimo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Dk. Soud Nahodha Hassan, alisema kwa upande wa Zanzibar asilimia 60 ya kilimo kinachofanyika visiwani humo ni kilimo hai.

"Na sisi wizara tunajipanga kwa mwaka wa fedha tutaiweka bajeti ya kuendeleza kilimo hai Zanzibar kwa sababu tunaona umuhimu wake.

Nimefarijika pia kuona huku Bara nako watu wanakitaka kilimo hai," alisema Dk. Soud.

Awali, akimkaribisha mgeni rasmi, Mwenyekiti wa Taasisi ya Kilimo Hai Tanzania (TOAM), Dk. Mwatima Juma, alisema kongamano hilo la siku mbili linawaleta pamoja wadau wa kilimo hai na serikali kujadili masuala mbalimbali yatakayoinua kilimo hicho.

# Waziri ataja sababu makandarasi wazawa kunyimwa kazi za serikali

**Na Paul Mabeja**, DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, ametaja baadhi ya mambo yanayosababisha makandarasi wazawa kunyimwa kazi kuwa ni pamoja na wizi wa fedha za miradi na kufanya kazi chini ya kiwango.

Kutokana na hali hiyo, amewataka kuacha kulalamika kuwa wananyimwa kazi badala yake waonyeshe ufanisi kwenye miradi mbalimbali wanayopewa ili kujenga uaminifu.

Simbachawene aliyasema hayo juzi alipokuwa akifungua mkutano wa 10 wa mwaka wa Chama cha Makandarasi Wazalendo Tanzania (ACCT).

Alisema moja kati ya kero katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ni makandarasi wengi kushindwa kukamilisha miradi kwa wakati na kwa ubora uliokusudiwa.

"Baadhi yao wakipewa kazi za serikali, wanasubiri malipo ya awali ambayo badala ya kufanyia kazi, wanaanza kununua magari ya familia halafu mwisho wanalalama kwamba miradi haiwasaidii kitu kumbe ni tofauti," alisema.

Waziri Simbachawane alisema moja ya sababu ambazo ziliifanya serikali kuacha kuwatumia makandarasi na kutumia mfumo wa 'force account' ni miradi mingi kutekelezwa kwa gharama kubwa lakini ikiwa chini ya viwango.

"Matumizi ya 'force account' yamefanya makubwa lakini pia bado yana changamoto zake, hivyo makandarasi tunatakiwa kubadilika ili kila mmoja wetu atimize wajibu wake. Serikali ina mapungufu (upungufu) yake (wake) lakini pia nyie mna mapungufu (upungufu( yenu (wenu)," alisema.

Alisema serikali hiyo inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan, inayo dhamira ya dhati kujenga sekta binafsi yenye nguvu.

"Yaliyopita si ndwele tugange yajayo. Mmezungumzia kuhusu malipo lakini kiukweli hivi sasa serikali tunalipa lakini ni ninyi mnapaswa kubadilika sana katika kutekeleza majukumu yenu ya kila siku.

"Hivi sasa ukiangalia wale wanaojenga reli ya mwendokasi (SGR), unakuta daraja kubwa na refu lakini ndani ya muda mfupi limekamilika lakini akipewa mzawa hapa hata daraja la milioni moja tu mtasubiri hadi kukamilika siyo leo," alisema.

Pia aliwataka makandarasi wazawa kujifunza kwa wageni namna ambavyo wanasimamia miradi wanayopewa na serikali ikiwemo ujenzi wa SGR na mingine mingi.

"Leo hii ukikuta mkandarasi mzawa anajenga daraja utakuta kaweka vigunia kwa ajili ya kumwagilia maji lakini hawa wenzetu hata huoni hivi vigunia au maji wanamwagilia muda gani lazima tujiulize ni teknolijia ipi wanatumia tofauti na sisi ili tujifunze," alisisitiza.

Mwenyekiti wa ACCT, Thobias Kyambo, alisema miradi mingi ya serikali inawaumiza na kuwafilisi makandarasi wazawa kutokana na kutolipwa kwa wakati.

Aliiomba serikali kuja na utaratibu mwingine kama ilivyo kwa mataifa mengine mfano Uingereza ambako mkandarasi anajenga na kulipwa kwa wakati.

Alisema Tanzania kuna utaratibu wa kupewa kazi halafu mkandarasi anakopa na kujenga na akimaliza halipwi kwa wakati, hivyo anabaki kuwa masikini.



Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima (kulia), akikata utepe kuzindua kitabu cha mwongozo wa kutoa elimu ya afya ya macho kwa makundi mbalimbali nchini, kilichoandaliwa na wizara hiyo, katika maadhimisho ya Siku ya Afya ya Macho Duniani, iliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma juzi. Kushoto ni Mkurungenzi wa Magonjwa yasiyoambukiza wa Wizara hiyo, Dk. James Kiologwe. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAMISEMI yaonya walimu kubambikiwa makosa

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imepiga marufuku walimu kubambikiziwa makosa ili kukwamishwa kupandishwa madaraja.

Naibu Waziri wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI, David Silinde, alilipiga marufuku hiyo juzi jijini hapa alipokuwa akifungua kikao kazi cha Makaimu Makatibu Wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kutoka Wilaya 139.

Alisema kumekuwa na tabia ya kuwabambikia makosa mbalimbali walimu ili wasionekane watendaji wazuri, jambo linalowakwamisha kwenye upandishaji wa madaraja.

"Sitaki kusikia walimu wanabambikiwa makosa na makatibu kwa kuwa inachangia kumkosesha mwalimu nafasi ya kupandishwa daraja. Ikibainika hatua zitachukuliwa," alisema Silinde.

Pia alisema hakuna sababu ya kuweka uadui na walimu na kuwataka kuepuka vitendo vya rushwa wakati wa kupendekeza majina yao kupandishwa madaraja.

"Nawapongeza suala la kupandisha walimu madaraja lakini nasisitiza rushwa iachwe kwa walimu wenye sifa wapewe nafasi ya kupandishwa madaraja,"alisisitiza.

Silinde alisema suala la rushwa halipaswi kuingizwa kazini, hivyo nivyema wakaliacha na kuwapa nafasi walimu kufanya kazi kwa bidii bila makandokando yoyote.

Aliwataka kushiriki ipasavyo kwenye utekelezaji wa miradi ya elimu ambayo fedha zake zilitolewa na serikali hivi karibuni kupitia mkopo wa masharti nafuu kutoka Shirika la Fedha Duniani (IMF).

Silinde alisema TAMISEMI ilipatiwa mgawo wa mkopo huo Sh. bilioni 536.6 kati ya Sh. trilioni 1.3 na kati ya hizo, Sh. bilioni 304 zimepelekwa kwenye miradi ya elimu.

Pia alizitaka Halmashauri kuhakikisha zinawapatia walimu Ofisi zenye hadhi ya kufanyia kazi na si kuwaacha wakifanya kazi katika mazingira ambayo hayastahili.

Alisema Ofisi yake itaangalia suala la bajeti ili

kuhakikisha wanafanya kazi katika mazingira yenye weledi ambayo yatamfanya mwalimu kufanya kazi yake kwa weledi mkubwa.





# SMZ yachukua tahadhari corona kwa watalii

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema inachukua tahadhari zote kuhusu ugonjwa wa corona kwa wageni wakiwamo watalii wanaoingia nchini ili kuwa salama baada ya kupata chanjo zilizothibitishwa na Shirika la Afya Duniani (WHO).

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi, Rahma Kassim Ali, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu ujio wa idadi kubwa ya watalii kutoka mashirika mbalimbali ya ndege duniani.

Alisema watalii wanaowasili Zanzibar wote tayari wamefuata utaratibu unaotakiwa kufuatwa ikiwamo kupimwa afya na chanjo ya kujikinga na corona.

Rahma alisema mashirika yote ya ndege ya kimataifa yanayoleta wageni, yanatakiwa kufuata masharti hayo na kuhakikisha watalii wote wanapata chanjo ya kujikinga na corona zilizothibitishwa na WHO.

"Watalii wote wanaokuja nchini tunahakikisha wanafuata utaratibu wa afya na mojawapo ni kupata chanjo ya corona kwa mujibu wa masharti ya WHO," alisema.

Aidha, alisema kundi la watalii 172 waliowasili Zanzibar hivi karibuni kwa ndege ya shirika la ndege la Ufaransa, wote wamefuata utaratibu wote wa kupata chanjo zilizothibitishwa na WHO.

Naye Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto Nassor, Ahmed Mazrui, alisema vituo vyote vikuu vinavyopokea wageni ukiwamo Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume, Bandari ya Malindi wameweka wafanyakazi wanaoangalia masuala ya chanjo.

Alisema suala la chanjo kwa watalii wanaoingia nchini limepewa kipaumbele cha kwanza kuhakikisha hakuna maambukizi yanayoweza kuletwa na wageni.

Aidha Mazrui alifurahishwa na baadhi ya hoteli kubwa zinazopokea watalii nchini kuona wafanyakazi wake wote wamepata chanjo kujikinga na ugonjwa huo pamoja na kuwakinga wageni.



Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud (katikati aliyekaa) akiwa katika picha ya pamoja na viongozi wa jumuiya ya kupambana na dawa za kulevya na UKIMWI (ZAYADESA), alipoitembelea jumuiya hiyo, Mazizini Mjini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Othman akemea ushirikiano wa matukio

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema ushirikiano kati ya wadau na serikali katika vita dhidi ya dawa za kulevya na UKIMWI usitegemee matukio na ziara za viongozi na badala yake uwe mikakati na mipango ya pamoja ili kuyakabili vyema matatizo hayo.

Othman aliyasema hayo jana alipozungumza na uongozi wa Jumuiya ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Ukiwmi (ZYEDESA), alipotembelea ofisi za jumuiya hiyo, Mazizini Wilaya ya Magharib 'B,' Unguja.

Alisema kuwapo kwa hatua hiyo ni muhimu katika kurahisisha utekelezaji wa juhudi za pamoja za mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuzuia maambukizi mapya ya UKIMWI ili kuwa na jamii bora yenye uwezo wa kuchangia maendeleo ya taifa lao.

Pia alisema mipango ya serikali na wadau kuhusu vita hivyo ikijumuishwa kwa pamoja ni rahisi kutekelezwa vyema na Zanzibar kufikia ipasavyo utekelezaji wa malengo ya nchi na hatimaye kutimiza matarajio ya taifa ya kuondokana na dawa za kulevya na maambukizi ya mapya ya UKIMWI.

Alisema kwamba utaratibu huo pia unasaidia kuepusha migogano katika utekelezaji wa mipango na mikakati ya mapambano dhidi ya UKIMWI na dawa za kulevya na kuweka mustakabali sahihi wa malengo ya nchi katika mipango ya maendeleo.

Othman alipongeza mchango mkubwa unaotolewa na ZYEDESA katika mapambano hayo na kusema serikali ya Zanzibar inaunga mkono ipasavyo juhudi hizo za pamoja kwa kuwa wamekuwa na ujasiri wa kuyakabili masuala mbalimbali kwa uwazi jambo ambalo limesaidia sana kuwepo mafanikio mkubwa zaidi hivi sasa.

Kuhusu mazingira, Othman aliwapongeza wanajumuiya hiyo kwa uamuzi wao wa kuliingiza suala hilo kama sehemu ya utamaduni wa jamii, jambo ambalo litasaidia uhifadhi bora wa mazingira Zanzibar.

Alisema kuna nchi nyingi duniani kutokana na jitihada za pamoja za kuhifadhi mazingira, zimeyageuza majangwa kwenye nchi zao kuwa misitu lakini Zanzibar ni kinyume, hivyo kasi ya ukataji miti imegeuza misitu kuwa majangwa jambo ambalo limechangia uharibifu mkubwa wa mazingira.

Meneja Miradi wa ZYEDESA, Lusian Mgole, alisema jumuiya hiyo imekuwa ikisaidia katika vita dhidi ya UKIMWI ili kupata tiba sahihi na kuendelea kubaki kuwa salama.

Alisema jumuiya hiyo kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imetenga vituo tofauti Unguja na Pemba ili kutoa huduma kwa vijana na wanawake zitokanazo na matatizo ya dawa za kulevya na virusi vya UKIMWI (VVU).

# Polisi mguu sawa kukabili uhalifu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JESHI la Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, limesema limeweka mkakati madhubuti wa kuwakamata watuhumiwa wa matukio mbalimbali ya kihalifu ikiwamo uvunjifu wa amani, wizi na udhalilishaji ili kupunguza matukio hayo katika mkoa huo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mjini Magharibi, Omar Said Nassir, alisema jana kuwa mkakati huo utawashirikisha viongozi wa shehia kwa kushirikiana na wananchi ambao watawafichua wahalifu.

Alisema watakapowabaini wahalifu hao kupitia taarifa mbalimbali ikiwamo kwa raia wema na viongozi wa shehia, watawakamata na watakaobainika na hatia watafikishwa katika vyombo vya sheria.

"Tukishawakamata kulingana na kesi zao watakaokutwa na ushahidi tutawapeleka mahakamani na watakaokuwa kwa siku ile hawajapatikana tutawaangalia ambapo wengine utakuta ni wahalifu lakini ushahidi kupatikana kwake unakuwa mgumu kidogo hivyo atakuwa anaripoti kwa wiki mara moja," alisema.

Pia alisema mkakati mwengine ni kupeleleza kesi kwa umakini na kwa haraka na kwamba zilizopo kwa sasa wanazipitia kwa kuangalia upelelezi wake ukoje na kusawazisha upungufu uliokuwapo kwa kuyatolea marekebisho ili upelelezi wao kwenda kwa umakini, usahihi na kwa uharaka zaidi.

"Kazi hii tutaendelea kushirikiana kwa karibu zaidi na masheha, raia wema na wananchi kwa ujumla ili kutupatia taarifa za kiuhalifu kwa sababu watuhumiwa wengi wanaingia miongoni mwa jamii, hivyo sisi polisi tupo karibu na jamii kwani hawa ndio wanaowafahamu zaidi," alisema.

"Kama kuna raia mwema anamjua mhalifu na anaogopa kutoa taarifa zake kwa kuhofiwa kutajwa, nawaomba mnipe mimi moja kwa moja. Taarifa hizo tutazitunza na hazitotoka na kwa kiasi kutomfanya mtu kuogopa kwa kuhofia maisha yake labda akitoa taarifa zake polisi zitafika kwa mhalifu," alisema.

Kuhusu hali ya usalama kimkoa, Kamanda Nassir alisema kwa sasa hali inaridhisha isipokuwa kumekuwapo udhalilishaji ambapo jamii imepata mshituko ya kuwa makosa yameongezeka sana.

Alisema uwazi aliouweka Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, wa kulipiga vita suala la udhalilishaji, uimesaidia jamii kupata uelewa na mwamko wa kwenda kuripoti kesi hizo katika vyombo vya sheria.



# LINEX

UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
JUMAMOSI OKTOBA 23, 2021



# Diamond Mungu anakuona ujue

HUYU ndiyo Diamond Platnumz bwana. Kwanza kabisa akiwa nchini Marekani alitoa dongo la mwaka akiwataka wasanii wa Tanzania wanaotaka kufanya shoo nchini humo kwanza watoe ngoma za maana ili waende huko wakajaze mashabiki na si kupigia viti au ukumbi mtupu.

Wakati mashabiki wa muziki wakitafakari, akachaguliwa kuwania tuzo za MTV Europe Musica Awards (MTV EMA) 2021 kwenye kipengele cha Best African Act.

Diamond alijirekodi akisema maneno haya "Mkija huku mfanye mambo ya maana, kwanza toeni nyimbo mkija huku mjaze."

Maneno hayo yakawa gumzo kwenye mitandao ya kijamii, kila mtu akisema yake, wengine wakisema kuwa ni dongo kwa baadhi ya wasanii.

Hivi karibuni baadhi ya wasanii wa Bongo Fleva walikwenda nchini Marekani, lakini inadaiwa hawakufanikiwa kujaza ukumbi, badala yake video zilizopigwa na kuwekwa kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha kuwa kulikuwa na watu wachache tu ukumbini.

Lakini yote hayo yamekatishwa na msanii huyo kuchaguliwa kwenye tuzo hiyo. Sasa stori zimebadilika, watu wanazungumzia tuzo hiyo.

Atachuana na wasanii wengine wanne kutoka Afrika ambao ni Tems wa Nigeria, Wizkid wa Nigeria, Focalistic wa Afrika Kusini na Amaarae wa Ghana.

Sherehe za kutangaza tuzo hizo zitakuwa Novemba 14. Ni tuzo ambayo pia itawashirikisha wasanii mbalimbali wakubwa wa kimataifa kutoka nchi mbalimbali duniani, kwenye vipengele tofauti.

Baadhi yao ni kama vile Doja Cat, Ed Sheeran, Justin Bieber, Lady Gaga, Lil Nas X, The Weeknd, Pop Bora kwenye kipengele cha msanii bora. Zaidi ya vipengele sita vitakuwa vinagombaniwa.

BASI SAWA

## Linex kumbe mtabiri aisee



MSANII Linex kama mtabiri vile. Amesema huko nyuma aliwahi kulalamika kuwa muziki wa kizazi kipya umeingiliwa na muziki wa staili nyingine ya amapiano, akiwataka wasanii wenzake kuachana na muziki huo utawaharibia, lakini hawakumsikia.

"Nilishawahi kulizungumzia hili huko nyuma watu wakaja juu. Lakini hao hao hivi sasa ndiyo wanalalamika. Mimi nililiona hilo kabla wao hawajaliona, sasa ndiyo wameliona," alisema Linex.

Anasema kwa sasa yeye hazungumzi tena. Alishasema zamani, wakamuona namna gani vipi, sasa basi.

"Mimi sisemi kitu kwa sasa. Mtu akiimba madogoli sawa, mimi ninachotaka ni kufanya muziki wangu tu, sitaki kumzungumzia yoyote. Kila mtu afanye anachojisikia kufanya, mradi tu anaona unamlipa na anawafurahisha mashabiki wake", amesema.

## Asha Boko mumeo kijana inawahuu?



JAMANI ikifika mwezi ujao ndoa ya mwigizaji wa filamu kawaida na zile za vichekesho, Asha Boko, inatimiza mwaka.

Mwenyewe Boko na mumewe Dua Msafiri wanapendana kama wameoana jana vile.

Amesema baada ya ndoa kuna watu walikuwa wanamwambia eti mbona ameolewa na mwanaume kijana.

"Hadi leo kuna watu wanadhani kuwa mume wangu ni kijana. Mume wangu siyo kijana, ila ana mwili mwembamba tu huyu," amesema Boko.

Amesema anashukuru Mungu kumkutanisha na mwanamume kama huyo na walikutana kama utani vile.

"Tulikutana kwenye sherehe moja hivi. Tulionana, lakini kila mtu alikuwa kivyake, si unajua kwenye shughuli. He, tukakutana stendi. Mimi natafuta bajaj ya kwenda Tegeta Nyuki na yeye pia. Nikamkumbuka, nikamwita. Si unajua tena Mungu akipanga lake. Nikamwambia kama unakwenda Nyuki panda humu. Tukabadilishana namba."



## Kipara cha Mziwanda elfu 40

KUNA watu anatumia wembe wa Sh. mia au mia mbili tu kunyoa nywele zote kichwani na kuwa kipara.

Siyo kwa mwanamitindo Chris Mziwanda. Kwa mdomo wake mwenyewe anadai kuwa yeye akienda saluni anatumia Sh. 40,000 kunyoa nywele kwa mtindo wa kipara. Habakishi chochote kichwani.

Halafu anafanya hivyo kila baada ya siku mbili.

Hii inasababishwa na mwonekano wake mpya ambao anataka kuwa nao na aina yake ya maisha kuwa ya gharama kiasi kwamba akijifikiria hata mwenyewe huwa anajiogopa.

## Kifo cha Siri: Utapoteza vyote, damu haipotei

**Na Adam Fungamwango**

KIFO cha siri ni filamu inayoonyesha jinsi binadamu anavyoweza kufanya kila kitu kupoteza ushahidi baada ya kufanya uhalifu, ikiwamo kuua mtu, lakini ni ngumu kutoacha alama yoyote.

Waswahili wana msemo usemao 'damu haipotei', ikiwa na maana yeyote anayeweza kumuua biandamu mwenzake na kumfukia, au kumtupa popote pale hata kama ni baharini, ipo siku itakuja kugundulika tu, hata kama baada ya miaka mingi kupita.

Wacha-Mungu nao wana msemo wao kuwa 'damu inaomwagika bila hatia ni lazima imlilie Mungu na atanyoosha mkono wake, ili mwovu apatikane'. Ndiyo atapatikana hata kama atajitahidi kutoacha alama.

Moni na Mona ni mabinti wawili mapacha. Wanafanana na korosho. Moni ambaye ni doto anasoma shule ya sekondari, kurwa wake Mona, yeye alishaacha zamani. Labda shule haipandi. Hawa wasichana wanalelewa na bibi yao, kwani mama yao walifariki wakati wakijifungua.

Moni anaingia kwenye mahusiano ya kimapenzi na kijana Surej. Mapenzi yanampovusha na safari za kwenda shule zinapungua. Anavaa unifomu, akifika njiani anageuza njia kwenda kwa Surej.

Siku moja anabambwa na kijana mmoja anayeitwa Amos. Kijana huyo baadaye anakutana na Mona kisimani. Anaanza kumwambia yale yote aliyoyaona. Anampa vipande yake kuwa badala ya kwenda shule anakwenda kwa mabwana. Hakujua kuwa anayemwambia ni Mona na si Moni. Pamoja na kushangaa, Mona anabeba na kuyapeleka kwa bibi yake. Naye anashindwa kuelewa nini kimetokea. Mona anakuwa na wasiwasi na ndugu yake Moni. Siku moja anaibamba simu. Anamwambia bibi yake. Simu inapigwa mbele yake. Bibi anamlazimisha kuiweka kitufe cha kuongeza sauti. Inasikika sauti ya mwanaume, akizungumza maneno ya mapenzi, ikionyesha ni wapenzi wa muda mrefu. Moni anapata mkong'oto unaomfanya kukimbia nyumbani. Anakimbilia kwa Surej. Bahati mbaya tayari ni mjamzito huku akiwa ni mwanafunzi. Hilo



linamtisha mno Surej. Anaomba ushauri kwa rafiki yake.

Moni anaanza kuumwa tumbo. Kutokana na kukosa huduma bora na lishe, anafariki dunia. Surej na rafiki yake wanachoamua ni kwenda kumzika usiku bila mtu kujua. Ambacho walikuwa hawaelewi ni kwamba rafiki wa Surej alikuwa na mdogo wake mwenye umri wa miaka saba, ambaye aliona kila kitu.

Mtoto huyo baada ya siku mbili anakutana na Mona, anamshangaa. Mona anamuuliza kwa nini anamshangaa, akamjibu kuwa anachokijuwa yeye ni kwamba aliumwa tumbo, akafa anazikwa kwenye shimo, lakini leo anamuona yuko hai. Siri inafichuka. Mona anakwenda kuwaambia bibi yake na majirani. Polisi nao anafika. Mwili unafukuliwa. Mtoto anasema ni nani wanahusika. Surej na rafiki yake wanakamatwa.





## Kflow ana kwikwi

MSANII wa muziki nchini Tanzania, Kflow ametangaza kuachia EP yake ya kwanza mwaka huu iitwayo 'Kachumbari' itakayokuwa na idadi ya nyimbo sita.

Kflow alithibitisha hilo na kuongeza kuwa baada ya EP hiyo ya nyimbo zilizo kwenye mtindo wa sauti tupu, maarufu kama 'audio' mpango unaofuata ni kuziachia kwa njia ya video.

Amesema kuwa katika albam hiyo, kuna bonge moja la ngoma linaitwa 'kwikwi' ambalo ana uhakika litatesa kinoma kwenye televisheni, redio na mitandao ya kijamii.

Amesema kuwa uzinduzi wa albamu hiyo utafanyika hivi karibuni baada ya kukamilika albamu zote mbili upande wa 'audio' na 'video'.

Amezitaja ngoma hizo kuwa ni 'Mafuriko', 'OG', 'Tamba', 'Kwikwi' , 'Tell Me' na 'Sinyorita.'.

## WATU NA ALBAM ZAO MWAKA HUU

**Na Adam Fungamwango**

HIVI majuzi tu msanii Ali Kiba ameipua albam mpya kabisa, ambayo mwenyewe ameipa jina la 'Ony One King'. Imeanza kusumbua kwenye vyombo mbalimbali na mitandao ya kijamii. Ni albam yenye pini 16 za kufa mtu.

Kwa muziki wa bongo fleva ulivyo, si rahisi sana kwa msanii kutoa albam. Inatakiwa machozi, jasho na damu kuweza kufanya hivyo. Wengi wao huishia kutoa singo tu, ili kama zikifanya vema wapate mialiko kwenye shoo. Ndiyo maana utauona kwa mwaka mzima, siyo wasanii wengi wanaotoa na wala huwezi kuona idadi kubwa ya albam.

Mpaka kufikia Oktoba mwaka huu ni wasanii wachache, ambao wamefanikiwa kufanya hivyo. Nao ni hawa hapa, tukianza na Kiba mwenyewe.

**Ali Kiba 'Only One King'**

Ni albamu matata ambayo amewashirikisha wasanii kibao kutoka ndani na nje ya nchi, wakiwamo Sauti Sol, Rude Boy, Mayourkun, Nyakishinksi, Sarkodie na wengine wengi. Ina ngoma 16.

Nazo ni 'Oya Oya', 'Amour', 'Tamba', 'Sitaki Tena', 'Salute', 'Washa', 'Infidele', 'Bwana Mdogo', na 'Habibty', Wengine ni 'Gimme Dat', 'Niteke', 'Let Me', 'Utu', 'Ndombolo', na 'Happy'.

**Mbosso 'Definition Of Love'**

Msanii mwingine ambaye mwaka huu hajapoa ni Mbosso. Huyo alichomoka na albam, ambayo aliipa jina la Definition Of Love.'

Yeye alikuwa na pini 12 za hatari. Nazo ni 'Kiss me', 'Baikoko', na 'Karibi' alizomshirikisha Diamond Platnumz, 'Tulizana', ambayo ameiimba na Kilimanjari Connection 'Wana Njene', 'Yallah, 'Sakata', 'Pakua', 'Your Love', 'Kadada', 'Yes' na 'Nipo Naye.'

**Rayvanny 'Sounds From Afrika'**

Ni albam ya aina yake ambayo imefyatuliwa na msanii Rayvanny yenye vitu 23 vya maana.

Kuna ngoma iliyobeba jina la albam inayoitwa 'Sounds Of Afrika', 'Tetema', akishirikisha 'Diamond', 'Senorita', 'Kelebe', 'Chuchuma', 'Tingisha', ' Number One Remix', na 'Juju'.

Pini zingine kali ni 'Koroga', 'Rotate', 'Bebe', 'Baby', 'Bailando,' 'Twerk', 'Zuwena', 'Lala', 'Mama', 'Kiuno', 'Marry Me', 'Zamani', 'Waongo', 'Juu' na 'Woza'.

**Rapcha 'Wanangu 99'**

Rapcha naye ni mmoja wa wasanii waliotoa albam zao mwaka huu. Yeye albamu yake yenye ngoma nane tu, ameiita 'Wanangu 99.'


Pini hizo ni 'Majani', 'Go Baba', 'Unajua Vibe Remix', 'Nitakucheki', 'Kama unaye', 'Tunajimwaga', 'Wanangu', 'Lisa' namba moja na namba mbili.


**Best Naso 'Gift of Life'**

Huyu ni mwimbaji wa nyimbo za kunung'unika na kulalamika. Yeye mwaka huu naye hakuwa nyuma. Ana albam yake inaitwa 'Gift Of Life', yenye ngoma 31.

nazo ni 'Walikuwepo', 'Dola', 'Usitoe', 'Kaza Moyo', 'Avera', 'I Know', 'Mrudie Dada Yangu', 'Twanga', 'Utabamba', 'Mkia', 'Miti Miti', 'Oh Nah', 'Kwa Huku', 'Hidaya', 'Hellena', na "Maringo'.

Zingine ni 'Nyonga', 'Afrika', 'Matoleo', 'Anko', 'Wanawake', 'Amelia', 'Mapenzi', 'Tamba', 'Nitomase', 'Baunsa', 'Asu', 'Mshenga', 'Fumanizi la Baba', 'Mke wa Kuoa', 'Mama', na 'Twanga Remix'.





## Davido ona mtoto alivyowaunganisha

MWANAMUZIKI wa Nigeria, Davido na mchumba wake wa muda mrefu Chioma, wameungana tena katika sherehe ya kutimiza miaka miwili ya mtoto wao wa kiume, Ifeanyi.

Wawili hao waliweka picha na ujumbe katika akaunti zao za intagram zikiwaonyesha wana furaha kwa mtoto wao.

Naitakia furaha siku yako ya kuzaliwa mtoto wangu David Ifeanyichukwu Adedeji Adeleke, ukiwa mkubwa utakuwa maarufu zaidi yangu," ameandika Davido.



## Alec hujajua bunduki haina huruma

MWIGIZAJI maarufu wa Marekani, Alec Baldwin, ameingia matatani baada ya kusababisha ajali na kuua mwanamke mmoja wakati wakiigiza filamu.

Kulingana na ripoti ya uhakika msanii huyo alifyatua risasi wakati wa uchukuaji picha na bahati mbaya ilimpiga mwongozaji na kumjeruhi vibaya.

Tukio hilo limetokea kipindi ikitumika bunduki katika mji wa Mexico wakati inarekodiwa filamu ya Rus


## Medikal umeyataka mwenyewe

MSANII wa Ghana, Medikal, anashikiliwa na polisi baada ya kuonyesha bunduki katika mtandao wa kijamii.

Medikal, pamoja na mkewe Fella Makafui, wanashikiliwa makao makuu ya polisi mjini Accra kwa ajili ya mahojiano.

Katika video fupi msanii huyo alionekana akitoa maelekezo kuhusu silaha yake aina ya bastola jambo lililozua taharuki kwa jamii.





## Kanye West Ye usituharibie watoto

MMEMUONA Kanye West alivyonyoa? Huyu anaweza kabisa kutuharibia vijana wetu na watoto. Rapa huyu na mfanyabiashara kutoka Marekani, ameendelea kuutikisa ulimwengu kwa aina yake ya mitindo mbalimbali ya mavazi, viatu, na sasa ameibuka na mwonekano mpya wa nywele.

Rapa huyo ambaye kwa sasa amejibatiza jina jipya la Ye, ameshea picha yake ya mtindo huo mpya wa unyoaji kwenye mtandao wa kijamii na ambao umezua gumzo kubwa.

Wapo wanaouliza ni nani kinyozi wake aliyebuni mtindo huo. Mnyoo huo umewachengua wengi ulioonekana baada ya kuvua maski yake kichwani ambayo aliivaa kwa muda mrefu.

## R Kelly kweli unataka kujitundika?

MWANAMUZIKI mwimbaji wa R&B wa Marekani R. Kelly ilibidi awekewe uangalizi maalum akiwa gerezani kwa hofu ya kujiua mwenyewe kutokana na msongo wa mawazo.

Mwanasheria wa mwimbaji huyo Steba Greenberg, amethibitisha kuwa Kelly aliwekewa uangalizi maalum na wa kina akiwa gerezani baada ya kukutwa na makosa ya kujihusisha na biashara ya ngono na unyanyasaji wa kijinsia kwa hofu ya kujiua.

Hata hivyo anasema hivi sasa imeaondolewa baada ya kukutwa na hatia na hukumu yake inatarajiwa kusombwa mwezi Mei 2022.

Wanasheria wanadai kuwa kwa makosa hayo, anaweza kupigwa mvua 20, hadi kifungo cha maisha.



MAKALA

# Washindi kesi wanavyopigania marufuku mabinti kuolewa ianze kutekelezwa sasa

## •Kilio chao sasa ni mabadiliko ya kisheria
## •Walioozeshwa wasimulia 'madudu' kwao

**Na Elizabeth Zaya**

SUALA la Sheria ya Ndoa nchini, kimsingi imekuwa mjadala mkali ambao umechukua muda mrefu, mzizi wa malalamiko ukijikita katika kipengele kinachoruhusu binti wa umri mdogo kuruhusiwa kutolewa

Wapo waliohama kutoka nadharia na kufuata msukumo wa kisheria, wakiwa na mafanikio. Hata hivyo, mzizi wa malalamiko sasa uko katika hatua ya mbele zaidi ya mafanikio hayo, utekelezaji wa uamuzi wa mahakama.

Shirika la Msichana Initiative, linasisitiza mamlaka zinazohusika na kutunga sheria kuleta mabadiliko katika baadhi ya vifungu vya Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 iliyohusu msichana wa umri miaka 14 kuolewa. Mahakama ilibatilisha.

Shirika hilo kupitia mkurugenzi wake, Rebecca Gyumi, lilifungua shauri katika Mahakama Kuu ya Tanzania kwa niaba ya watoto wote walio hatarini kuingia kwenye ndoa za utotoni, dhidi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, kupinga uhalali wa sheria ya ndoa za utotoni.

Rebecca alishinda shauri kwamba Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 ina walakini kwa kukinzana na katiba ya nchi, akirejea vifungu viwili vya sheria anavyodai vinakiuka ibara ya katiba ya nchi, katika mtazamo wa haki na usawa wa watu, pia kwenye kijinsia.

Ndoa za utotoni husababisha athari mbaya za kiafya, kiuchumi na kijamii na kwa mujibu wa ripoti inayohusika na Idadi ya Watu na Maendeleo ya Afya (TDHS) ya mwaka 2015/016, inayoonyesha wasichana wawili kati ya watano au sawa na asilimia 63 Tanzania, wanaolewa chini ya miaka 18.

Takwimu zinaonyesha, Mkoa wa Shinyanga unaongoza kwa asilimia 59 ya ndoa za utotoni, ukifuatiwa na Tabora (58), Mara (55) na Dodoma asilimia 51.



Wasichana, kundi linalohitaji uangalizi maalum kufikia malengo yao, ikiwamo jamii kuwalinda kimasomo. Pichani, wakiwa katika nyendo tofauti zinazoendana na maisha yao ya shule. **PICHA ZOTE: MAKTABA**

### HUKUMU INAVYONENA

Hukumu hiyo ya mahakama ta Julai mwaka 2016, ilitamka ndoa yoyote ya mtu mwenye umri chini ya miaka 18 ni kinyume cha sheria, kwa kuwa hazitoi usawa kwa msichana na mvulana katika njia mbili.

Kwanza, kuna angalizo la umri wa ndoa ni tofauti kati yao. Pili, wasichana wenye umri chini ya miaka 18, wanahitaji ridhaa ya wazazi kuolewa, wakati wavulana hawahitaji ridhaa ya namna hiyo ya mzazi, hali inayoonyesha kutokuwapo haki sawa.

Serikali ilipokata rufani kupitia shauri la mwaka 2017, bado mahakama ilimpatia ushindi Rebeca, ikitoa mwaka mmoja sheria hiyo iwe imefanyiwa marekebisho.

Rebecca anasema, pamoja na hukumu kutolewa na mahakama bado haridhishwi na hatua zinazochukuliwa kufanikisha marekebisho ya kisheria.

"Tunajivunia kama shirika kutumia jukwaa letu kuhamasisha mabadiliko ya sheria hii, iliyokuwa inaruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa.

"Tunaishukuru Mahakama ya Rufani kupitia hukumu ya rufani, ambayo ilibatilisha vifungu hivyo. Kwetu sisi ni mafanikio makubwa sana," anasema Rebeca.

Hata hivyo, anakiri mbali na ushindi huo wa kisheria, kuna kazi kubwa ya kuhakikisha muswada wa kubadili sheria hiyo unafikishwa bungeni, ili kuendana na adhabu kwa mtu anayemuoza binti wa umri chini ya miaka 18.

"Tunatamani kuona mchakato wa mabadiliko ya sheria ya ndoa unakamilika mapema iwezekanavyo, ili kuendana na maelekezo yaliyotolewa na mahakama ya rufani na kuongeza ulinzi kwa watoto wanaopitia ukatili huu," anasema.

Rebeca anashauri mamlaka ziheshimu uamuzi uliotolewa na mahakama kwa kufanya marekebisho ya sheria hiyo haraka kubatilisha vifungu hivyo, ili kuliokoa kundi la watoto wa kike ambao ndio waathirika wakubwa.

### WAHUSIKA WAELEZA

Jema Sabugo, mkazi wa Bahi mkoani Dodoma, ni miongoni mwa wanaofanya kazi na Shirika la Msichana Initiative kutoa elimu ya kukomesha ndoa hizo za utotoni, anasema baadhi ya familia bado zinaishikilia kuoza mabinti wadogo wakigeuza ndio njia ya kujipatia mtaji.

"Tunakumbana na visa na mikasa vingi sana, lakini tunachobaini ni kwamba wazazi ni miongoni mwa watu wanaochangia kuendelea kuwapo kwa ndio hizi za utotoni.

"Wapo baadhi yao wanaoamini kwamba ukibahatika kuzaa mtoto wa kike, umepata mali. Wanafanya kama biashara, wanaona wamepata utajiri, wamepata ng`ombe," anaeleza

Clementina (jina la pili tunalo), mkazi wa Bahi mkoani Dodoma, anadokeza kuwa aliozeshwa ndoa ya kimila na wazazi wake alipokuwa na umri miaka 15, baada ya kuachishwa shule.

Hata hivyo, anasema ndoa yake ilidumu kwa siku mbili tu baada ya polisi ilipomkamata na mume wake, akiwa na ufafanuzi: "Siku ya tatu, polisi wakaja kutukamata na kutupeleka kituo cha polisi.

"Tulipofika kule, askari walimwambia mume wangu kwamba ameoa mtoto ambaye alitakiwa kuwa shuleni na wakaanza kuwatafuta wazazi wangu. Kuanzia hapo ndoa ikawa imevunjika.

"Mimi nilifurahia kitendo cha polisi kutukamata, kwa sababu nililazimishwa kuolewa na yule mwanamume kwa sababu tu alikuwa amelipa mahali kwa wazazi wangu na nilikuwa natamani kuendelea na shule."

Mwingine mwenye mkasa unaofanana, ni Monica (jina lingine tunalo) mkazi wa mkoani Shinyanga, anasema wazazi wake walikataa kumwandikisha shule, lakini alipofikia umri miaka 12, alijipeleka mweye pamoja na mdogo wake kwenda kujiandikisha.

Monica anasema, wazazi wake hawakufurahia wao kwenda shuleni, hivyo walihakikisha siku za shule wanawapeleka kuchunga ng`ombe, pamoja na shughuli za nyumbani, hivyo wakajikuta wanaacha shule ndani ya miaka miwili; darasa la pili.

"Wazazi wetu waligoma kutupeleka shuleni mimi na mdogo wangu, lakini baadaye nilipofika umri wa miaka 12 nilijipeleka mwenyewe shuleni pamoja na mdogo wangu.

"Nilipofikia umri wa miaka 14, nikatafutiwa mwanamume wa kunioa, akaja nyumbani wakatufungisha ndoa ya kimila," anasimulia Monica..



## ILIVYOKUWA ZAMANI, LEO & YAJAYO

# Unajua namna vitongoji maarufu vya Dar vilikoanzia? Pata darasa!

**Na Adam Fungamwango**

DAR ES SALAAM inajulikana kuwa mji mkubwa kuliko yote nchini, bara na visiwani. Cha ziada ndani yake kuna vitongoji vingi vinazaliwa kila kukicha.

Maana yake ni kwamba, hata kulikokuwa ama porini au shamba zama hizo, leo hii ni jiji tena 'pamekucha' kwa kila kitu.

Ni katikati ya miaka ya 1970 wakati huo muziki wa dansi umelishikilia jiji na taifa kwa jumla, bendi ya kiwanda maarufu cha nguo (Urafiki Textiles), Urafiki Jazz Band iliibuka na wimbo kuhamasisha Operesheni Vijiji vya Ujamaa, iliyoanza mwaka 1974.

Watu walitakiwa kuhamia penye vijiji vya Ujamaa kama vile ambavyo mwimbaji alivitaja kwa kujinasibu akigani kupataja; Gezaulole, Kibugumo, Mwanadilatu, wakati huo kukiwa wilayani Temeke, lakini sasa ni Kigamboni, hali kadhalika Tegeta ikidumu wilayani Kinondoni.

Leo hii yakitoka maelezo ya hilo la vijiji kutekelezwa, huenda ikaonekana uchulo, maana kote huko ni mjini hasa, tena viwanja havipatikani na vikipatikana, bei yake ni ya juu sana. Mitaa imeshamiri, aduika na wakazi lukuki.

Pia, waliokuwa watoto na wazaliwa na hata mashuhuda wake zama hizo, sasa ni watu wazima wameshavuka zama za ujana na baadhi wazee.

Ni simulizi inayoenda mbali mtu akipaita kwingine kama Mbezi katika barabara ya Morogoro nako 'shambani' huku maeneo kama Buza na Madale kulikuwa shamba, lakini sasa ni mjini na hasa kunapanuka.

Leo hii shinikizo la mjini kupanuka kumeibua wilaya mpya kama Kigamboni na Ubungo, jumla yake kuwa tano kutoka tatu za wakati huo.

Kwanza, kwa swali ni wangapi wanafahamu mkoa wa Pwani haukuwapo na badala yake ilikuwa sehemu ya Dar es Salaam na Mkuranga sehemu ya Wilaya Kisarawe?

Hata hivyo, ndani ya maeneo kongwe, yana simulizi na mzizi wa umaarufu wake. Kuna vitongoji maarufu kwa majina yake hadi sasa, ikianzia na mzizi ya kilichojiri wakati huo.

Wapo wanaopakumbuka Msasani wakati huo, pakiwa kitongoji wakazi wake wengi sana walikuwa jamii ya Wamakonde, ambao kutokana na lafudhi yao walimuita mtu maarufu wa mahali hapo 'Mussa Hassani' wenye wakaangukia matamshi 'Mchachani' na umma ukangukia majumuishi ya kauli 'Msasani.'

Lakini, hapo hapo tena, kuna mtaa marufu unaoitwa 'Maandazi Road' zao la foleni ndefu ya vibatari vya wauiza maandazi mahali hapo usiku, hata pakajijengea umaarufu na leo ni jina rasmi, sasa ikitimu zaidi ya miaka 40.

Hisitoria kama hiyo ndio imeifikia eneo Chang'ombe Unubini, jirani kwa mitaa michache kutoka palipo sasa panakoitwa Chang' ombe Mchichani, ambako muda mrefu waliishi jamii kabila la Wanubi kutoka Sudan (sasa Sudani Kusini) kabla ya Uhuru.

Umbali mfupi pana eneo maarufu 'Chang'ombe Maduka Mawili'. Unajua kwanini jina hilo? Kabla katikati ya miaka 1970, mahali hapo kulikuwapo duka moja kongwe maarufu 'Changa Store' tangu zama miaka ya 1960, ikiwa pekee, majirani wa mbali, nyumba zilizomilikiwa na serikali, Posta na binafsi za 'uhindini.'

Ndipo kukafunguliwa duka lingine mshindani wakati huo, liitwalo Chang'ombe Store (sasa mgahawa) ambalo lilionekana zuri sana, hata kuipiku Changa Store iliyokuwa maarufu kwa kuuza mikate adimu kutoka wazalishaji waliokuwapo jirani 'White Heart Bakery'.

Chang'ombe wakawapiku kwa mikate mipya ya kisasa 'Siha' iliyozalishwa na Shirika la Usagishaji la Taifa (NMC), pia mikate mingine ya Gloria, ambayo ilizalishwa eneo la keko.

Mara moja kwa jumla, mahali hapo pakawa maarufu, ikaongezwa na mabasi mapya aina ya Ikarus yenye tela, kama ya sasa kwenye Mwendokasi, kukapafanya hapo mahali pa kugeuzia.



Sehemu ya mitaa ya Yombo Buza, Dar es Salaam, ikiwa katika maendeleo, miongo minne iliyopita ilikuwa pori.


Eneo kongwe la Majumba Sita, kipande cha Ukonga ambacho kimedumu kuwa mjini miaka mingi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Mara moja mahali hapo mji mzima kakavuma kwa jina Maduka Mawili, linalodumu hadi sasa, licha ya majengio kuongezeka.

Pia, umbali mfupi kutoka hapo kuna 'Keko Bora' ambayo ni zao la kuwapo fremu iliyokuwa na maduka matano maarufu, kunakoishia Mtaa wa Ngomati (Nyuma ya TCC klabu).

Ni mahali palikuwapo duka la viatu vya kampuni ya Bora, Duka la Ushirika Cosata, wakati huo, ushirika maduka yake yalikuwa maarufu sana, ndiko vitu muhimu vilipatikana tena kwa foleni na siku maalum. Nayo ikahalalisha kituo kuelekea mahali hapo kudumu kwa jina Bora hadi sasa.

Kwingineko ni Buza, ambako kulidumu kuwa shamba kwa miaka mingi, mji ukishia Tandika. Baada ya jiji kiuanza kutanuka mwishoni mwa miaka ya 1980, kulianzishwa baa iliyojulikana Lulenge, ikimilikwa na mwenyeji wa asili ya Mkoa Kagera. Moja kwa moja kubatizwa jina la Kwa Lulenge, lialotamba hadi sasa.

Ni aina ya majina ambayo ndio yatawala maeneo ya Ukonga Banana, ambako kuna njia panda ya kwenda Kitunda. Mzizi wake ni kuwapo baa maarufu Banana, iliyodumu hadi mwanzoni mwa miaka ya 1990 ilipouzwa, sasa kukishuhudiwa kituo kikubwa cha mafuta.

Kutoa hapo Banana, umbali wa vituo vitatu kuelekea Gongolamboto, panapojulikana Ukonga Mombasa, inaasiswa na kuwapo baa iloyoitwa kwa jina hilo, tangu zama hizo pakiwa 'nusu shamba.'

Mahali hapo kuna kituo jirani nako kunajulikana Ukonga Madafu, jina likitokana na kuwapo biashara maarufu ya madafu tangu miaka michache ya uhuru, pakiwa shamba nje ya Jiji la Dar es Salaam, kukitenganishwa na Mombasa, kwa kambi ya Polisi wa Kutuliza Ghasia (FFU).

Eneo ambako lilikuwa kama ukingo mji kwa njia hiyo ni penye umaarufu hadi sasa kwa jina Ukonga Majumba Sita, kituo kimoja kutoka uwanja wa ndege, kuelekea porini Gongolamboto.

Kwa nini majumba sita? Ni kutokana mahali hapo kambo ya ndege za jeshi, ambako jirani na barabarani, sasa pamejengwa ukuta na kuna nyumba za sita za maofisa wa jeshi tangu zama za ukoloni, hata ikapabatiza jina hilo.

Kwingineko ni Magomeni, ambako kuna bibi anatajwa alikuwa maarufu kwa kufuga paka wengi, naye akajikuta mahali pake panapewa jina la Kwa Bibio Nyau, huku Mbezi kulikuwapo makazi ya kiongozi mwanadamizi wa jeshi, kukaitwa 'Mbezi kwa Msuguri', Kijitonyama Makumbusho na Mwananyamala kwa Kopa.

Ni dhana inayotawala hata mikoa mingine, maana hata jijini Mbeya, kulikuwapo muuzaji kinywaji maarufu Mama John, ameacha umaarufu wa jina la eneo, licha ya sasa hayuko tena, lakini umaarufu huo umedumu.

Naam! Ndivyo, maisha ya jana, leo na tuendako na yanayojiri, Usikose Jumamosi ijayo, kuendelea na kidodoso kingine cha jiji la Dar es Salaam.

**Mawasiliano ya ujumbe: +255 716350534 au barua pepe: afungamwango@gmail.com**

HABARI KIMATAIFA

# Shirika la reli Nigeria lasitisha huduma

**ABUJA,** NIGERIA

SHIRIKA la reli la Nigeria limesitisha kwa muda huduma za reli kutoka Abuja, kuelekea kaskazini magharibi mwa Kaduna baada ya watu wenye silaha kuwavamia abiria kwenye treni siku ya Jumatano.

Watu walioshuhudia walisema washambuliaji hao walimlenga dereva wa treni ingawa hakuna majeruhi aliyeripotiwa mpaka sasa.

Abiria mmoja aliiambia BBC kuwa walisikia mlio mkubwa kabla ya treni haijasimama kwa saa kadhaa.

Mbunge wa zamani nchini humo, Seneta Shehu Sani, aliandika kwenye ukurasa wa tweeter kuwa ni treni ya pili na hivyo kulazimika kurudi Abuja siku ya Alhamisi baada ya mlipuko ulipotokea katika reli hiyo.

Kampuni ya reli ya Nigeria ilisema huduma hizo zitarudi Ijumaa baada ya ukarabati. **BBC**

# Wanafunzi walivamia bunge DRC wakitaka walimu wao waongezewe mshahara

**KINSHASA,** DRC KONGO

MAMIA ya wanafunzi wamelivamia bunge nchini DRC wakitaka walimu wao waongezewe mshahara.

Wanafunzi hao walikuwa wanapeperusha matawi na kuimba "tunataka kusoma" na "ikiwa hatutasoma, tutatumia dawa za kulevya".

Maandamano ya aina hiyohiyo yalitokea katika mji wa Beni kaskazini mwa Kivu ,kwa mujibu wa redio inayomilikiwa na Umoja Mataifa- Radio Okapi.

Walimu wamekuwa katika mgomo tangu Oktoba 4, mwanzoni mwa masomo mwaka huu wakitaka waongezewe mshahara na kupunguza umri wa kustaafu pamoja na masuala mengine.

Serikali imewashutumu viongozi wa dini ambao wanasimamia shule nyingi za msingi, kuwa wanahusika na mgomo huo ingawa viongozi hao wamekanusha madai dhidi yao.

Makamu wa Rais wa Jamhuri ya demokrasia ya Kongo, Jean-Marc Kabunda, amewataka wanafunzi kurudi nyumbani kwa kuwa hayo sio mapambano yao.

"Nyinyi sio watu wa mtaani, mnapaswa kuwa shuleni na kama hampo shule mnapaswa kuwa nyumbani," alisema.. **BBC**

# Wabunge wahalalisha utoaji mimba Benin

**PORTO NOVO,** BENIN

WABUNGE nchini Benin wamepiga kura kuhalalisha utoaji mimba na kuongeza wigo wa jambo hilo ambalo tayari lilikuwa likifanyika.

Wanawake sasa wanaweza kutoa mimba katika miezi mitatu ya mwanzo ya ujauzito iwapo kama ujauzito huo utamsababishia shida katika masuala ya elimu, kazi, maadili au mtoto anaweza kuathiri maisha ya mama au kwa ajili ya maslahi ya mtoto.

Hapo kabla utoaji mimba ulikuwa unaruhusiwa kisheria endapo mwanamke alibakwa au maisha ya mama yalikuwa hatarini kwa sababu ya ujauzito.

Benin ilikuwa inaruhusu utoaji mimba kama afya ya mtoto ambaye hajazaliwa itaathirika.

Sheria mpya, ilipitishwa Jumatano usiku baada ya majadiliano makali bungeni , lakini bado katiba inapaswa kupitishwa mahakamani kabla ya utekelezaji kuanza.

Waziri wa afya, Benjamin Hounkpatin, ameunga mkono sheria hiyo mpya na kusema itaweza kuleta haueni kwa wanawake wengi ambao wanapata ujauzito wasioutaka na hivyo kutafuta njia hatari zinazohatarisha maisha yao ili kutoa mimba.

"Nchini Benin, karibu wanawake 200 wanakufa kila mwaka baada ya kupata matatizo wakati wa kutoa ujauzito ," alisema. **BBC**



Wabunge nchini Benin wakiwa bungeni wakati wa upigaji kura kuhalalisha utoaji mimba. **PICHA BBC**

# Marekani yasema itaitetea Taiwan shambulio la China

**NEW YORK,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden, amesema nchi yake itaitetea Taiwan ikiwa Uchina itashambulia, hatua ambayo inatofautiana na sera ya muda mrefu ya Marekani

"Ndio, tuna wajibu wa kufanya hivyo," alisema alipoulizwa katika ukumbi wa mji iwapo Marekani itailinda Taiwan .

Msemaji wa Ikulu baadaye alivieleza baadhi ya vyombo vya habari vya Marekani kwamba matamshi yake hayakuashiria mabadiliko ya sera.

Marekani kwa muda mrefu imekuwa ikifanya "utata wa kimkakati" linapokuja suala mwiba wa kutetea Taiwan.

Hii inamaanisha kuwa Marekani imekuwa na msimamo wenye utata kwa makusudi juu ya kile itakachofanya ikiwa China itashambulia kisiwa hicho.

Marekani haina uhusiano wowote wa kidiplomasia na Taiwan, lakini inauza silaha kwa kisiwa hicho kama sehemu ya Sheria ya Uhusiano ya Taiwan, ambayo inasema kuwa lazima iisaidie Taiwan kujilinda .

China inaiona Taiwan kama jimbo lililojitenga, ambalo linaweza kuchukuliwa tena kwa nguvu siku moja ikiwa ni lazima, wakati Taiwan inadai kuwa ni nchi huru.

Mvutano umekuwa ukiongezeka kati ya nchi hizo mbili katika wiki za hivi karibuni baada ya Beijing kurusha ndege kadhaa za kivita katika eneo la ulinzi wa anga la Taiwan. Utawala wa Rais Joe Biden uliidhinisha mauzo mengine ya kibiashara ya moja kwa moja kwa Taiwan tangu achukue madaraka mapema 2021 na imetaka kuimarisha uhusiano zaidi na kisiwa hicho, na kusababisha hasira kutoka Beijing. **BBC**

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## MAGARI

**GARI INAUZWA,** AINA YA VOLKSWAGEN TOUREG YA MWAKA 2004 NAMBA DDV RANGI NYEUSI. INATEMBEA NA IKO KWENYE HALI NZURI SANA. BEI NI TSH. 15,000,000/- PIGA SIMU NAMBA 0762 810 451.

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

## KUPOTEA KWA CHETI



**KHAMISUU KOMBO YASINI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.1437/0014** kilichotolewa na **FILBERT BAYI SEKONDARI** mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/URA/RB/505810/2021.**

116527002

## KUPOTEA KWA CHETI



**BRIDGITH CHRISTOPHER MUSHI** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3948/0010** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ENDUIMET SEKONDARI** mwaka 2020. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya Polisi: **ARU/ARU/RB/488838/2021.**

116526602

## KUPOTEA KWA CHETI CHA CHUO



**AYUBU MCHOMVU** anatangaza kupotelewa na cheti cha Chuo chenye namba **BSc ICT-B 103040102-14** kilichotolewa na **CHUO KIKUU CHA MZUMBE** mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **WMB/RB/482/2021.**

116526802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA.1/2020**
**(Asilia shauri la jinai Na.82/2018, Mahakama ya Wilaya Mtwara)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA..........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**HAMISI MOHAMED @NAUDENDE............. MJIBU RUFANI**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA:HAMISI MOHAMED@NAUDENDE**
**NAMNYAMBA**
**MTWARA**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA RUFAA HII MNAMO TAREHE 17/11/2021 SAA 2:30 BILA KUKOSA.

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA BASI RUFAA HII ITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA WEWE KUWEPO.

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 06/10/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

116522802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84)**

**Mahakama ya Mwanzo ya ILALA**
**Wilaya ya ILALA**

**MADAI NAMBARI 130 YA 2021**

**Mdai NEW RAINBOW AFRICA LIMITED**

**amdai**

**Mdaiwa SUPER SIP LTD (INOCENT KIMATI)**

**Kwa kuwa mdai/wadai/ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba**

**FIKA BILA KUKOSA KUJA KUJIBU MADAI YA TSH. 17,045,550/**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya ALHAMISI tarehe 28/10/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo. Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo **tarehe................ 20/20.**

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO
ILALA - WILAYA YA ILALA

116527902

## KUPOTEA KWA CHETI



**SHABAN M. HUSSEIN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S.0765/0502** kilichotolewa na UNYANYEMBE HIGH SCHOOL mwaka 2021. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/505564/2021.**

116528202

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ISSA DADI NDOVU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 198 DRW.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SO/RB/2021.**

116527502

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SWALEHE ASEDI SHAWEJI** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 539 ADH.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya Polisi: **SO/RB/2021.**

116527402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA: 63)**

**Mahakama ya mwanzo ya ..........MJINI...-...TANGA**
**Wilaya ya ............................TANGA**

**MADAI NAMBARI....62....ya 2021**

**Mdai ...................SAMIRI ABDULHAMANI LADHA**

**Mdaiwa................SALIMU ATHUMANI KIGOWELA**
**Kwa: ..............SALIMU ATHUMANI KIGOWELA**
**.........c/o .....MW/KITI..... PONGWE**

**Kwa kuwa mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI TA TSHS 14,025,000/=**

Kwa hiyo unahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMATATU 01/11/2021 saa 2:30 asubuhi kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo ni lazima kuleta mashahidi wako na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.
Angalia kama hukuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, Mahakama ikithibitisha kama umepokeakuitwa shauri hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo 25/10/2021.

25/10/2021

116527302

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**JUDICIARY**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**AT BUKOBA**

**MISC.LAND CASE APPEL NO. 25 OF 2021**
**(Originating from application No. 142 of 2016 DLHT Bukoba & Civil Case**
**(No. 15 of 2013 Kahororo Ward Tribunal)**

**JULIUS RWECHUNGURA .................................. APPELLANT**

**VERSUS**

**JEREMIAH MRAMBA NYAKABI ..................RESPONDENT**

**TO: JEREMIAH MRAMBA NYAKABI**

**RE: NOTICE OF DATE OF HEARING.**

Whereas the above mentioned appellant lodged Appeal against your and registered as Misc. Land Appeal No. 25 of 2021.
Take notice that the above said case has been fixed for hearing on 27/10/2021 at 8:30am before Hon. Emmanuel L. Ngigwana, Judge you are authorized to appeal in person or through your advocate.
Take further notice that in default of your appearance on that date time for the said hearing the case will proceed in your absence.
Given under my hand and seal of the court this ............day of.............

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
BUKOBA

1167527202

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**EVANCE BRIGHTON MUNISHI** anatangaza kupotelewa na Result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S4213/0557** iliyotolewa na MARIAN BOYS HIGH SCHOOL mwaka 2021. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.Taarifa ya polisi: **DAR/CHU/RB/503960/2021.**

1165283302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

**Simu: +255 26 2324455**
**Fax: +255 26 2323233**
**Baruapepe: ps@mow.go.tz**
**Tovuti: www.mwtc.go.tz**

**Mtaawa Moshi,**
**S.L.P 2888,**
**40470 DODOMA**
**Tarehe 23/10/2021**

## TANGAZO

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **JUMATATU** tarehe **25/10/2021** kampuni ya **LOGISTICS FOR SUB SAHARA** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **TUNDUMA** kuelekea **MTUKULA** gari hilo lenye namba za usajili: **410 SSC FS / 232 SSC FS.**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | **-** | **mita** | **22.00 M** |
| **Upana** | **-** | **mita** | **4.40 M** |
| **Kimo** | **-** | **mita** | **4.85 M** |

3. Njia itakayotumika: **TUNDUMA hadi MTUKULA Kupitia MIKUMI, gari litasafiri muda wa mchana tu (Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

1167527102

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**EXPENSIANA ARKADI TESHA** anatangaza kupotea kwa kadi yake ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 653 CCE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/504233/2021.**

116527702

**JAMHURi YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**FORM II**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa mirathi NA. 94/2021**

**Ombi la FATUMA E. NDEKILO kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu RAMADHAN SALUM MARIJANI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII POPOTE ALIPO**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 26-10-2021 kabla ya muombaji kuteuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 13/10/2021

Tarehe 13/10/2021
Sahihi ya Hakimu

116527602

**THE REGISTRATION OF DOCUMENTS ACT(CAP 117)**
**DEED POLL ON CHANGE OF NAMES:**

By this DEED POLL I, **FLORENTINA ANDREW SARGA,** a Citizen of the United Republic of Tanzania, of P**ostal Address Box Number 383, Babati-Manyara, Tanzania,** DO HERBY wholly relinquish and abondon the use of my former names of **FLORENTINA ANDREW NAANO,** and adopt as from the date of this Deed poll and in substitution of my former names, the names of **FLORENTINA ANDREW SARGA.**

That, for the purpose of Evidence of such determination, **I HEREBY DECLARE** that, I shall at all times hereinafter in all records, deeds documents and other writings and in all actions and proceedings as well as in all Public and Private dealings and transactions and, for all occasions whatsoever use and subscribe the said names **FLORENTINA ANDREW SARGA.**

**AND I HEREBY** expressly authorize and reguire all and every person whomsoever at all times after the date hereof to designate, describe and address me by the adopted names of **FLORENTINA ANDREW SARGA.**

**IN WITNESS WHEREOF,** I have set my **HAND** at Babati-Manyara, and hereon substitutes my former names of **LUCIA DEEMAY SULLEY,** with my current or new names of **FLORENTINA ANDREW SARGA.**

SWORN at BABATI by the said FLORENTINA ANDREW SARGA, who is known to me personally in my presence this **5th day of October 2021.**

116528602

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**REDEMPTA JOHN MBATIA,** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari , Yenye namba za usajili **T 608 AKK LANDROVER** Chassis namba **SAL L JGMF7MA094798,** Engine namba **18L05403A** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **KIL/MOS/RB/505017/2021**

116528502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**OMARY M. MAKUNGANYA** Anatangaza kwa kupotelewa kwa kadi yake ya pikipiki aina yake **SUNLG** yenye usajili namba **MC 502 AXF CHASSIS NO.LBRSPJB51A9046240** Kwa yeyote atakae ona au kuokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **Rb Namba. MOR/MOR/RB/501086/2021**

116528702

**OFISI ZA MATANGAZO**

**Mikocheni Industial Area,**

**Po.Box 31042, Dar es Salaam. Mob: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.
Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake amekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.
Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka Mke Wangu-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**




Alimhadithia Tedi kwa ufupi. Hakujua kama Tedi anafahamu kila kitu. Anamfahamu hadi Sam. Na si mgeni hapa Morogoro, ila ni mwenyeji ambaye alikuwa anafanya kazi ya uhudumu wa baa, ingawa kwa sasa Tom amemsimamisha na kumtawisha.

"Sasa shoga, kwani hilo ni kosa lako? Wanawake wakati mwingine tunakwenda kuolewa na wanaume wengine na kuwaacha wapenzi wetu wengine ambao tulikuwa nao kwa muda mrefu. Cha kufanya si umuombe mumeo msamaha?"

"Hapana, kwanza hata kama yeye atakubali, sidhani kama ndugu zake wanaweza kukubali. Pili Sam mwenyewe bado yupo, anaweza kufanya chochote kile."

Wakati wakiongea, Tedi alikuwa anawasiliana na Tom kwenye meseji. Ilikuwa ni saa 1:00 usiku. Mlango ukagongwa.

Ndugu mmoja wa Farida ndiye aliyekwenda kufungua. Wakati huo Farida na Tedi walikuwa wanaendelea kujadiliana.

Aliingia mgeni. Ni mgeni aliyesababisha kila mmoja ndani kushtuka, kasoro mmoja tu.

Alikuwa ni mwanamume mwenye umri wa miaka 40. Mweusi, mwenye nywele nyingi kichwani, mrefu mwembamba. Hakuwa mgeni sana kwenye nyumba hiyo. Si mwingine ni Tom.

Ulikuwa ni mwendelezo wa mpango mkakati kati yake ya Tedi. Kati ya wote, Farida ndiyo alikuwa kwenye mshtuko mkali zaidi. Hakuwahi kumuona mumewe tangu alipomtoroka Dar es Salaam, wiki moja baada ya ndoa.

Ni kama vile halitaka kukimbia, lakini haikuwezekana. Miguu yake ni kama ilikosa nguvu ya kusimama ili akimbie. Hata midomo yake ilibaki kuchezacheza, huku sauti ikiwa haitoki.

Alikaribishwa ingawa kwa woga shemeji yake wa kike, mdogo wa mkewe. Aliingia kwa hatua za taratibu. Utulivu wake, na kutookena kwenye hali yoyote ya wasiwasi, ndiyo ilizidi mno kumtia wasiwasi Farida. Mdogo wake walitoka mbio nje. Nadhani kwenda kuita ndugu zake wengine ili kama kuna lolote baya waje kusaidia.

Bado Farida aliona ni kama anaota ndoto mbaya. hakujua atakapofika kwenye kochi, nini ambacho atafanywa. Mwili ulikufa ganzi. Sasa alikuwa tayari kwa chochote ambacho kitamkuta. Alitaka kutamka "nisamehe mume wangu". Lakini sauti bado ilishindwa kutoka kwa woga.

**"Unajua afande, kwa akili yangu nilijua kabisa nikisema ndiyo najikatia tiketi ya kuchwa. Mume wangu angejua kumbe nina mwanaume ambaye nilikuwa muda mrefu na ananikataza kuolewa. Hili sikutaka mtu afahamu."**

Tom hakuwa mgeni kwenye nyumba ile. Alikwenda kuketi kwenye kochi. "Habari zenu." Alisalimia, lakini aliyejibu ni Tedi. Farida bado alikuwa mbali kimawazo.

Muda mfupi baadaye ndugu wa Farida alirudi akiwa na ndugu zake wengine, ambao walikwenda kuitwa kwa kile kilichoonekana kama kunaweza kuzuka vurumai baada ya Tom kuingia.

"Hakuna ugomvi na wala hakutatokea kitu chochote, tumekuja hapa kuangalia nini kilitokea na nini cha kufanya ili kusuluhisha hili." Tedi alionekana kuwa kinara wa mazungumzo kuliko hata wanandoa wenyewe.

Tedi na Tom walimuonyesha Farida vielelezo vyote vinavyoonyesha kuwa alitoroka kutokana na kutishwa na Sam. Mpenzi wake wa zamani. Zilionyeshwa meseji zote walizokuwa wakitumiana Sam na Farida. Jinsi Sam alivyokuwa anamtisha kama akijaribu kuolewa na hata baada ya hapo, hali iliyomlazimu kuondoka kwa mumewe. Meseji zilikuwa kwenye simu ya Tedi. Alizitoka kwenye simu ya Sam aliyoichukua baada ya kumlevya.

Ilidizi kumshtua Farida. Hakuona jinsi yoyote ya kuongopa. Alijua huenda jambo lile lingejulikana. Lakini hakujua kama ingekuwa ni mapema vile. Alimsifu kimoyomoyo Tedi ambaye alidhani kuwa ndiye aligundua yote. Akili ikaanza kumtuma kuwa huenda alikuwa ni askari. Na yote waliyofanyika kumpigia simu na kuja pale nyumbani ilikuwa ni kupeleleza na kupata ukweli.

"Sasa kwa nini hukumwambia mumeo hilo swala ili kutafuta dawa ya kushikisha adabu mpaka ukatoroka kweli?" Tedi alimuuliza Farida.

"Unajua afande, kwa akili yangu nilijua kabisa nikisema ndiyo najikatia tiketi ya kuchwa. Mume wangu angejua kumbe nina mwanaume ambaye nilikuwa muda mrefu na ananikataza kuolewa. Hili sikutaka mtu afahamu."

"Sawa, sasa ulivyotoroka ulidhani kuwa ungekaa huko na muda gani, halafu ukarejea kwa mumeo?"

"Nilichanganyikiwa tu, yaani niliona bora kutoroka, baadaye ninaweza kufanya chochote na inawezekana nikarejea kwa mume wangu, kuliko picha zangu chafu kuonekana kwenye mitandao ya kijamii." Alipomaliza kuongea maneno hayo, Farida aliangua kilio.

Tedi na baadhi ya ndugu zake aliobaki hapo, baada ya kuona hakuna hali yoyote ya tafrani, bali ni mazungumzo tu ya kuwekana sawa, ndiyo walioanza kumbembeleza.

"Nisamehe mume wangu. Ni kweli kwa hili nimekukosea sana, ila mimi sikuwa na jinsi. Nilichokuwa natetea ni heshima yangu. Nisamehe nirudi nyumbani kwenye ndoa yangu."

"Una uhakika kuwa ukirudi, Sam hatochapisha tena hizo picha?" Tom aliongea kwa mara ya kwanza.

Aliuliza swali ambalo alikuwa na uhakika kuwa Sam asingeweza kufanya hivyo tena kwa sababu hana tena hiyo simu aliyokuwa anaitegemea. Farida hakujibu kitu.

"Kukusamehe au kutokukusamehe sitoweza kujibu hapa ghafla kiasi hiki. Naomba unipe muda, niende Dar. Nikae kwanza kama wiki moja, nijitafakari. Mimi sihofii ndugu wala rafiki, lakini nataka kwanza nitafakari, akili yake ikae sawa, ndiyo naweza kujibu."

*****************************

"Sasa uniachaje mpenzi? Tumeshamaliza mpango wetu. Wewe nipe nauli yangu ya kurudi kwetu Singida na ada yangu ya mwaka ya kwenye kusoma chuo cha urembo kama tulivyoahidiana."

"He mbona mapema hivyo?"

"Ndiyo, wewe si unakwenda Dar? Mimi hapa Moro natafutwa kama kipusa, nikionekana naweza kuuawa na Sam. Siwezi tena kurudia kazi ya uhudumu wa baa, wala kukaa hapa Moro. Na hii yote ni kwa sababu yako."

"Najua hilo mama."

"Unakumbuka nilikwambia kuwa nilikuwa nafanya kazi ile ili nicheze mchezo wa upatu, nilitimiza pesa ya ada, nakwenda kujiunga na chuo, nasoma huku nafanya kazi, nikihitimu naachana nayo."

"Ndiyo ni kweli. Na unakumbuka kuwa nilikwambia kuwa usifanye tena hiyo kazi?" Tom naye alimuuliza Tedi.

"Nakumbuka. Lakini si kwa sababu ya kazi hii na imekwisha, wewe si unarudi Dar kusubiria mambo yako na mkeo?"

Tom alicheka kicheko kifupi, halafu akamwambia "Kwani wewe hutaki kwenda Dar?"

"Kufanya nini ?"

"Si nilikwambia wewe umeshakuwa si mpenzi wangu tu. Ni mshauri wangu na rafiki yangu. Siwezi kuruhusu kukupoteza tena."

Tedi alimuangalia Tom kwa jicho la mshangao na mahaba kwa wakati mmoja.

"Mkeo je?" Akauliza.

"Alinitoroka."

"Anakusubiri umsamehe."

"Hata nikimsamehe siwezi kukuacha. Si unakumbuka tulisema utakuwa mke wa pili?" Tom alisema kwa utani.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AZAM, BIASHARA UNITED MAJARIBUNI UGENINI CAF

**Na Adam Fungamwango**

WAWAKILISHI wa Tanzania kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika, Azam FC, wanatarajia kushuka dimbani kuwakabili Pyramids katika mchezo wa marudiano wa michuano hiyo utakaochezwa leo nchini Misri.

Katika mechi ya kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam Jumamosi iliyopita, Azam ililazimishwa suluhu, hivyo itakuwa na kazi moja tu ya kusaka ushindi au sare ya magoli ili kusonga mbele katika michuano hiyo.

Timu itakayosonga mbele itakutana na klabu iliyotolewa katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa kucheza mechi moja ya mtoano na hatimaye mshindi atakuwa amefanikiwa kutinga hatua ya makundi.

Akizungumza na gazeti hili jana, nahodha wa Azam FC, Sospeter Bajana alisema wamejipanga kikamilifu kuwashangaza wenyeji wao ambao watakuwa wanatumia uwanja wa nyumbani.

Bajana alisema kila mchezaji amejiandaa kucheza kwa kiwango bora kwa sababu wanahitaji kusonga mbele kwenye michuano hiyo ya kimataifa ambayo hufanyika kila mwaka.

"Tumejiandaa kikamilifu. Kwa sasa tuna morali, hasa baada ya kushinda mechi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara. Tulikuwa tunautafuta sana ushindi. Ilikuwa inaniumiza mimi kama nahodha kukosa ushindi mechi tatu mfululizo, mbili za ligi na moja ya kimataifa na hawa hawa Pyramids. Lakini baada ya kuifunga Namungo FC imetuongezea ari, moyo na kiburi cha kupambana zaidi ili kuweza kupata matokeo mazuri tukianza na mechi hii," alisema Bajana. Naye mshambuliaji, Iddi Suleiman 'Nado' alisema wanatarajia mechi hiyo ya marudiano itakuwa na ushindani na wao kama wageni wamejiandaa kupambana ili kuondoka na ushindi.

Nado alisema wanawaheshimu wapinzani wao kutokana na historia nzuri waliyonayo kwenye michuano hiyo, lakini hawana presha ya mchezo huo wa marudiano.

"Ni mechi ngumu kama tulizocheza siku za nyuma, Waarabu wameanza kubadilika, hatuwaogopi, lakini tunajua matokeo ya kwanza yatakuwa yamewaweka njia panda wao pia, sisi wote tuna nafasi sawa, tutawashangaza,' alisema Nado.

Wakati huo huo, Biashara United kutoka Musoma mkoani Mara inatarajia kuwakabili wenyeji Al Ahly Tripoli katika mechi ya marudiano ya mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Biashara United inahitaji ushindi au sare ya aina yoyote ili kusonga mbele katika michuano hiyo baada ya kuwachapa wapinzani wao mabao 2-0 katika mchezo wa kwanza uliochezwa hapa jijini Dar es Salaam.




Baadhi ya wachezaji waliounda kikosi bora cha Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita wa mwaka 2020/2021. Kutoka kushoto ni Feisal Salum, Mukoko Tonombe, Dickson Job, John Bocco, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Shomari Kapombe na Aishi Manula. **PICHA: TFF**

# Twiga Stars matumaini kibao

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), kinatarajia kuwakabili wenyeji Namibia katika mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Dobsonville ulioko Soweto, Afrika Kusini.

Twiga Stars itashuka dimbani ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa mabao 2-1 katika mchezo wa kwanza uliochezwa Jumatano iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Kocha Msaidizi wa Twiga Stars, Edna Lema, aliliambia gazeti hili wamejiandaa vyema kuelekea mchezo huo na wamejipanga kupambana ili kusaka matokeo mazuri.

Edna alisema wamesharekebisha upungufu uliojitokeza katika mechi iliyopita na wamewafahamu vyema wapinzani wao.

"Tutapata matokeo, msiwe na wasiwasi, kama wao walishinda nyumbani, sisi pia tunauwezo wa kuwaondoa wakiwa kwao, inafungika, ninaamini hilo, " alisema kocha huyo.

Aliongeza anaamini Twiga Stars ina nafasi ya kusonga mbele endapo wachezaji wao watatekeleza maelekezo waliyowapa.

Namibia imelazimika kucheza mechi yake ya nyumbani nchini Afrika Kusini, baada ya uwanja wao kutokidhi vigezo.

## Nkongo afunguka TFF ilivyowabeba

**Na Shufaa Lyimo**

MKUFUNZI wa Waamuzi, Israel Nkongo amelishukuru Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa kuandaa mafunzo kwa waamuzi wa mchezo huo na kupelekea viwango vya waamuzi wanaochezesha mashindano mbalimbali hapa nchini kuimarika.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkongo alisema mafunzo hayo yanayotolewa yamewafanya waamuzi kutekeleza vyema majukumu yao na hivyo wamepunguza lawama mbalimbali zilizokuwa zinatolewa dhidi yao.

Nkongo alisema kwa sasa kelele dhidi ya waamuzi zimepungua kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa katika misimu iliyopita.

"Tunalishukuru Shirikisho la Soka hapa nchini kwa kutupa kozi mbalimbali ambazo zimesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza malalamiko yaliyokuwa yanatolewa kwa waamuzi," alisema Nkongo.

Mwamuzi huyo mstaafu wa kimataifa alisema TFF imefanya kazi kubwa kuhakikisha inaondoa tatizo hilo ambalo lilikuwa sugu huku pia likipelekea baadhi ya wachezaji kuona hawafanyiwi vitendo vya kiungwana wanapokuwa uwanjani.

Aliongeza anafurahi kuona ushindani umekuwa mkubwa katika Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu huku kila timu ikipambana kusaka wadhamini zaidi ili kusaidia shughuli za uendeshaji klabu hizo.

## Namungo, KMC mechi ya kiufundi

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Namungo inatarajia kuwakaribisha KMC FC katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Ilulu ulioko mkoani Lindi.

Kocha Mkuu wa Namungo, Hemed Morocco aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko tayari kwa mechi hiyo baada ya kurekebisha makosa waliyofanya katika mchezo wao uliopita.

Morocco alisema wamejipanga kuondoka na pointi tatu muhimu kwenye uwanja wao wa nyumbani ili kukaa kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo ambayo imeingia katika raundi ya nne.

"Tumejipanga vizuri kupata pointi tatu katika uwanja wetu wa nyumbani, makosa madogo madogo ambayo nimeyaona kwenye mchezo uliopita ninaamini hayatajirudia, tumeyaangalia na tumeyafanyia kazi, kwa sasa kila kitu kitakwenda vizuri," alisema Morocco. Kocha huyo alisema wachezaji wake wote wanaendelea vizuri na wameahidi watawapa furaha mashabiki wao ambao wamewaunga mkono wakati wote.

Mechi nyingine ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Shule ya Sekondari Nyankumu itakuwa ni kati ya wenyeji Geita Gold FC dhidi ya Mbeya City kutoka jijini Mbeya.

## ZISIKUPITE

### MADRID KUMKOSA HAALAND
REAL Madrid watamkosa mshambuliaji wa Borussia Dortmund, Erling Braut Haaland mwenye umri wa miaka 21, huku Manchester City, Paris St-Germain au Bayern Munich zikipewa nafasi ya kumnasa. **(AS)**

### UNITED, CHELSEA VITANI
MANCHESTER United na Chelsea zinamtaka pia Erling Haaland, ambaye anataka mshahara wa zaidi ya pauni milioni 30 kwa mwaka. **(ESPN)**

### TUCHEL AIVURUGA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund imekasirishwa na kitendo cha kocha wa Chelsea, Thomas Tuchel, kuzungumza hadharani kuhusu nia ya klabu yake ya kumsajili Erling Haaland mwenye umri wa miaka 21. **(Bild, via Mirror)**

### LINGARD ANUKIA EVERTON
EVERTON wanamtaka kiungo wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Jesse Lingard mwenye umri wa miaka 28 ifikapo dirisha dogo la Januari. **(Football Insider)**

### MBAPPE HUYO BARCA
BARCELONA inataka kuishinda Real Madrid katika mbio za kumsajili mshambuliaji wa PSG na Ufaransa, Kylian Mbappe, ambaye mkataba wake unamalizika mwishoni mwa msimu huu. **(AS)**

### DE BEEK KUONDOKA
KIUNGO wa Manchester United, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 24, hatarudi Ajax, lakini kuna uwezekano mkubwa ataondoka Old Trafford**. (Fabrizio Romano)**

### SOLSKJAER AFUNGUKA
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema klabu hiyo haijapokea ofa kutoka Everton kwa ajili ya kiungo wake wa Uholanzi, Donny van de Beek, licha ya kuwapo kwa tetesi nyingi. **(RTL7, via Manchester Evening News)**

### FATI ALIVIKACHA VIGOGO
LIVERPOOL, Manchester United na PSG walimpa ofa ya fedha nyingi, Ansu Fati ili ajiunge nazo kabla ya kinda huyo mwenye miaka 18 ambaye ni mzaliwa wa Guinea-Bissau, kusaini mkataba mpya na Barcelona. **(Cope)**

### CHIELLINI ATOA NENO
MLINZI wa Juventus, Giorgio Chiellini amesema ingekuwa bora zaidi mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 36, angeondoka mapema Juve na kujiunga na Manchester United. **(DAZN, via Goal)**

### WILSHERE KUTUA MAREKANI
KIUNGO wa zamani wa Arsenal na England, Jack Wilshere, mwenye umri wa miaka 29, yuko tayari kuhamia katika Ligi Kuu Marekani na anatajwa atajiunga na klabu ya Inter Miami. **(Talksport)**

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND ANOGESHA MBIO ZA UHAMISHO

## Afunguka kiasi cha mshahara anachohitaji kulipwa kama ataondoka Dortmund..

**DORTMUND, Ujerumani**

ERLING Haaland anahitaji kulipwa mshahara wa angalau pauni milioni 30 kwa mwaka kama ataondoka Borussia Dortmund na kusajiliwa klabu mpya wakati wa kipindi cha majira ya joto kijacho, kwa mujibu wa ESPN.

Manchester United, Manchester City, Chelsea na Real Madrid zote zipo kwenye mbio moja za kuwania huduma ya straika huyo wa kimataifa wa Norway.

Haaland mwenye umri wa miaka 21, anaweza kuondoka Dortmund mwishoni mwa msimu huu kama klabu mojawapo itafikia ada iliyowekwa ya euro milioni 75 ili kuondoka kwenye dimba la Signal Iduna Park.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo ya ESPN, Haaland anataka kulipwa pauni 500,000 kwa wiki katika klabu yoyote itakayomtaka.

Haaland alikataa kujiunga na Manchester United wakati wa kipindi cha majira ya baridi msimu wa 2019-20 na akaamua kutua Borussia Dortmund akitokea FC Salzburg.

Mwezi uliopita ESPN iliripoti Manchester United imefanya mawasiliano na Haaland ili kuangalia uwezekano wa kumsajili nyota huyo.

Kocha wa United, Ole Gunnar Solskjaer alijaribu kumshawishi kinda huyo ambaye alimnoa pale katika klabu ya Molde ya nchini Norway na bado anaendelea kufanya naye mawasiliano.

Haaland amefunga mabao 70 katika mechi 69 kwa Dortmund tangu alipojiunga na timu hiyo miaka miwili iliyopita.

Kabla ya kutua Ujerumani, alifunga mabao 29 katika mechi 27 alizoichezea Salzburg, ambapo alifunga 'hat trick' kwenye mchezo wake wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Genk ya Ubelgiji, Septemba, 2019.

Amefunga mabao 12 katika mechi 15 alizoichezea Norway na anaweza kuisaidia nchi hiyo kufuzu Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1998 kama itawafunga Latvia na Uholanzi kwenye mechi za mwisho za kufuzu zitakazochezwa mwezi ujao.


MECHI KALI
HOME
AWAY
BRIGHTON
6.92 | 4.39 | 1.46
MANCHESTER CITY

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 595

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# SOLSKJAER AFUNGUKA KUHUSU DE BEEK




**MANCHESTER, England**

OLE Gunnar Solskjaer anajua, Donny van de Beek "hana furaha" na "amechanganyikiwa" kwa kukosa nafasi ya kucheza katika kikosi cha Manchester United.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi aliwasili hapo akitokea Ajax kwa ada iliyoripotiwa kuwa pauni milioni 40 msimu uliopita, lakini nafasi ya kucheza pale Old Trafford imekuwa finyu kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24.

Van de Beek amecheza kwa dakika 140 kwenye mashindano yote msimu huu - dakika 90 kati ya hizo akicheza dhidi ya West Ham kwenye Kombe la Carabao na kiungo huyo alionekana na kamera za televisheni akionyesha kukasirika wakati akiwa benchi kwenye mchezo dhidi ya Villarreal mwezi uliopita.

Mchezaji huyo wa zamani wa Ajax alionekana kuitema jojo kwa hasira kwenye benchi la United wakati Jesse Lingard akiingia akitokea benchi.

Hata hivyo, alipoulizwa kuhusu tukio hilo baada ya ushindi dhidi ya Atalanta Solskjaer alitania kuwa hakuna shida, ingawa alikiri Van de Beek hana furaha.

"Ni jambo zuri kutema jojo na sio kumeza," alisema Solskjaer akiliambia gazeti la Uholanzi la RTL7. "Tulijifunza hivyo tulipokuwa watoto.

"Na kumpa jojo uliyotafuna mtu mwingine ni kitu kisichowezekana hasa wakati huu wa mlipuko wa corona. Hivyo niliona akitema mbali.

"Donny bado anajituma, bila shaka yoyote na wakati huu ni mgumu kwake na naelewa jinsi anavyojisikia hasa kwa kukosa kucheza mara kwa mara."

# Madrid, Bayern zamwania Rudiger



**LONDON, England**

REAL Madrid na Bayern Munich ni miongoni mwa timu kubwa Ulaya zinazojiamini zinaweza kumsajili, Antonio Rudiger wakati akiwa bado hajasaini mkataba mpya pale Chelsea, kwa mujibu ESPN.

Rudiger mwenye umri wa miaka 28, yupo kwenye mwaka wake wa mwisho pale Stamford Bridge, lakini mazungumzo kuhusu kuongezwa mkataba wake bado hajafanyika.

ESPN imeripoti kuwa Rudiger yupi tayari kubakia hapo na Chelsea bado wanahitaji huduma yake, lakini pande hizo mbili bado hazijafikia makubaliano.

Mlinzi huyo wa kati anataka mshahara wake kuongezwa mara mbili zaidi kutoka pauni 100,000 kwa wiki, huku Chelsea mwisho wao wa kuongeza ni pauni 150,000 kwa wiki.

Na hali hiyo imemfanya Rudiger kutokuwa tayari kusaini mkataba mpya na anaweza kuondoka kama mchezaji huru mwishoni mwa msimu huu.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, klabu kadhaa zimetoa ofa kwa Rudiger na zipo tayari kumpa mshahara wa pauni 300,000 kwa wiki kama ataondoka Chelsea.

Vyanzo zaidi vinadai Madrid, Bayern, Juventus na Paris Saint-Germain ni miongoni mwa timu ambazo zinafuatilia hali ya mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, ambaye amekuwa na kiwango bora tangu kuwasili kwa Thomas Tuchel mwanzoni mwa msimu huu.

Atakuwa huru kuzungumza na klabu yoyote kuanzia Januari mosi mwakani na hivi karibuni Rudiger mwenyewe alisema kuwa hana haraka kuhusu majaliwa yake.

HABARI MICHEZO


5,659,980 JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 23/10/2021 | 17:00 | Leeds vs Wolverhampton | 2.33 | 3.41 | 3.01 |
| 02. 23/10/2021 | 17:00 | Millwall vs Stoke City | 2.37 | 3.16 | 2.97 |
| 03. 23/10/2021 | 17:00 | Peterborough vs QPR | 2.90 | 3.20 | 2.39 |
| 04. 23/10/2021 | 17:15 | Cadiz CF vs Alaves | 2.51 | 3.02 | 3.07 |
| 05. 23/10/2021 | 19:30 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 3.02 | 2.82 |
| 06. 23/10/2021 | 22:00 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.53 | 3.14 | 2.93 |
| 07. 24/10/2021 | 14:00 | Nice vs Lyon | 2.63 | 3.47 | 2.53 |
| 08. 24/10/2021 | 16:00 | West Ham vs Tottenham | 2.38 | 3.36 | 2.96 |
| 09. 24/10/2021 | 16:00 | Brentford vs Leicester | 2.62 | 3.27 | 2.72 |
| 10. 24/10/2021 | 17:15 | Barcelona vs Real Madrid | 2.65 | 3.54 | 2.53 |
| 11. 24/10/2021 | 18:30 | Stuttgart vs Union Berlin | 2.36 | 3.44 | 2.84 |
| 12. 24/10/2021 | 18:30 | Manchester Utd vs Liverpool | 3.07 | 3.62 | 2.21 |
| 13. 24/10/2021 | 19:00 | Roma vs Napoli | 2.62 | 3.43 | 2.62 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE

"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 23 - OKTOBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 2875 | Chelsea vs Norwich City | 1.21 | 6.39 | 13.99 |
| 14:30 | 4392 | Cardiff vs Middlesbrough | 2.46 | 3.15 | 2.85 |
| 15:00 | 4179 | Valencia vs Mallorca | 1.70 | 3.78 | 4.93 |
| 16:00 | 2680 | Salernitana vs Empoli | 2.68 | 3.39 | 2.58 |
| 16:30 | 1839 | Arminia Bielefeld vs Borussia Dortmund | 7.38 | 5.19 | 1.36 |
| 16:30 | 2430 | VfL Wolfsburg vs SC Freiburg | 2.15 | 3.24 | 3.44 |
| 16:30 | 3529 | RB Leipzig vs Greuther Furth | 1.13 | 8.15 | 16.89 |
| 16:30 | 5738 | Bayern Munchen vs Hoffenheim | 1.16 | 8.16 | 11.94 |
| 17:00 | 1405 | Aberdeen vs Hibernian | 2.51 | 3.06 | 2.86 |
| 17:00 | 1503 | Leeds vs Wolverhampton | 2.56 | 3.31 | 2.76 |
| 17:00 | 1772 | Blackburn vs Reading | 1.88 | 3.45 | 3.94 |
| 17:00 | 2011 | Celtic vs St Johnstone | 1.23 | 5.90 | 10.82 |
| 17:00 | 2161 | Dundee Utd vs Motherwell | 2.27 | 3.25 | 3.05 |
| 17:00 | 2562 | Birmingham vs Swansea | 2.35 | 3.11 | 3.06 |
| 17:00 | 3228 | Queen of South vs Morton | 2.19 | 3.24 | 3.14 |
| 17:00 | 3316 | West Bromwich vs Bristol City | 1.42 | 4.34 | 7.10 |
| 17:00 | 3351 | Hearts vs Dundee FC | 1.45 | 4.24 | 6.70 |
| 17:00 | 3651 | Peterborough vs QPR | 3.30 | 3.50 | 2.06 |
| 17:00 | 3753 | Luton Town vs Hull City | 1.83 | 3.40 | 4.24 |
| 17:00 | 4103 | Millwall vs Stoke City | 2.53 | 3.07 | 2.83 |
| 17:00 | 4261 | Blackpool vs Preston | 2.38 | 3.15 | 2.96 |
| 17:00 | 4281 | Everton vs Watford | 1.65 | 3.91 | 5.22 |
| 17:00 | 4297 | Coventry vs Derby | 1.81 | 3.35 | 4.44 |
| 17:00 | 4644 | Ross County vs Livingston | 2.66 | 3.10 | 2.66 |
| 17:00 | 5176 | Crystal Palace vs Newcastle | 1.94 | 3.57 | 3.87 |
| 17:00 | 5178 | Southampton vs Burnley | 1.97 | 3.50 | 3.81 |
| 17:00 | 5456 | Viking vs Lillestrom | 1.89 | 3.84 | 3.50 |
| 17:00 | 5838 | Bournemouth vs Huddersfield | 1.66 | 3.70 | 4.94 |
| 17:15 | 5156 | Cercle Brugge vs Standard Liege | 2.51 | 3.34 | 2.65 |
| 17:15 | 5543 | Cadiz CF vs Alaves | 2.55 | 2.95 | 3.10 |
| 17:30 | 4733 | Santa Clara vs Famalicao | 2.44 | 3.16 | 2.87 |
| 18:00 | 2119 | Nantes vs Clermont Foot | 2.20 | 3.37 | 3.18 |
| 18:00 | 4247 | Wolfsberger AC vs Austria Klagenfurt | 1.66 | 3.72 | 4.45 |
| 18:00 | 5550 | Austria Vienna vs Josko Ried | 1.58 | 3.88 | 4.86 |
| 19:00 | 1594 | CSKA Moscow vs Kryliya Sovetov | 1.78 | 3.70 | 4.14 |
| 19:00 | 4478 | BSC Young Boys vs Lausanne-Sport | 1.19 | 6.68 | 11.80 |
| 19:00 | 5772 | Sassuolo vs Venezia | 1.60 | 4.33 | 5.03 |
| 19:30 | 1733 | Hertha BSC vs Monchengladbach | 3.58 | 3.63 | 1.96 |
| 19:30 | 2528 | Mechelen vs Zulte Waregem | 1.59 | 4.44 | 4.54 |
| 19:30 | 2985 | Elche vs Espanyol | 2.71 | 2.96 | 2.86 |
| 19:30 | 5938 | Brighton vs Manchester City | 6.92 | 4.39 | 1.46 |
| 19:45 | 3239 | Utrecht vs Heerenveen | 1.43 | 4.63 | 6.30 |
| 20:00 | 4897 | Tondela vs Porto | 7.33 | 4.95 | 1.36 |
| 21:00 | 1413 | PEC Zwolle vs Heracles Almelo | 2.81 | 3.36 | 2.37 |
| 21:30 | 3981 | Grasshoppers vs FC Zurich | 2.31 | 3.49 | 2.81 |
| 21:45 | 1949 | Bologna vs AC Milan | 3.38 | 3.58 | 2.09 |
| 21:45 | 3289 | Eupen vs Union Saint Gilloise | 3.75 | 3.75 | 1.85 |
| 22:00 | 4539 | Athletic Bilbao vs Villarreal | 2.49 | 3.11 | 3.01 |
| 22:00 | 4965 | Lille vs Brest | 1.57 | 3.99 | 5.58 |
| 22:30 | 4946 | Sporting Lisbon vs Moreirense | 1.24 | 5.70 | 10.82 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# FATI: JEZI YA MESSI HAINIPI PRESHA




**BARCELONA, Hispania**

KINDA wa Barcelona, Ansu Fati, amesema kuvaa jezi namba 10 ambayo ilikuwa inavaliwa na gwiji, Lionel Messi, haimpi presha kubwa.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania alizungumza kuhusu kufuata nyayo za Messi baada ya kusaini mkataba mpya ambao utamweka Barcelona hadi mwaka 2027 ambao unakipengele cha kuondoka kwa Euro bilioni moja.

"Ni kweli jezi namba 10 imekuwa ikivaliwa na Leo (Messi) na wachezaji wengine wengi, lakini mimi nimetulia," alisema Fati mwenye umri wa miaka 18, wakati akizungumza na waandishi wa habari.

"Najua nini ninachoweza kukileta kwenye timu. Kwa upande wangu sina presha kabisa.

"Hakuna mtu atakuwa kama Leo, hakuna mtu atakuwa kama nahodha wa zamani (Carles) Puyol au Xavi (Hernandez).

"Hakuna anayeweza kufikiria rekodi zilizowekwa na Leo. Nitakwenda safari yangu mwenyewe. Bado sijafanya chochote. Nina matumaini ninaweza kuwa na wakati mzuri wa kucheza hapa.

"Mchezaji yoyote anaweza kuvaa jezi namba 10, lakini ninachokiona ni kwamba hili ni jambo zuri zaidi kwangu."

# Arteta ana imani Lacazette kubaki




**LONDON, England**

MIKEL Arteta amekataa kuondoa uwezekano wa mkataba mpya kwa Alexandre Lacazette na amesema hajui chochote kuhusu molari ya mchezaji huyo wakati huu kukiwa na sintofahamu juu ya majaliwa yake.

Lacazette alitoka benchi na kuwasawazishia washikabunduki hao wakati wakifungana mabao 2-2 na Crystal Palace kwenye mchezo wa Ligi Kuu England, Jumatatu.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 mkataba wake wa sasa unamalizika mwishoni mwa msimu huu na atakuwa huru kuzungumza na klabu mpya, ifikapo Januari.

Hata hivyo, Arteta amesisitiza raia huyo wa Ufaransa bado anabakia kuwa mchezaji muhimu kwenye kikosi chake, akimsifia kwa kiwango bora dhidi ya Palace na ameacha milango wazi kuhusu ofa mpya.

Kwenye michuano yote pale Arsenal, Lacazette amefunga mabao matatu msimu huu (nyuma ya Aubameyang) na ametoa asisti moja katika dakika 185 alizocheza.

"Namtaka (Lacazette) kuendelea kufanya kile anachokifanya, alikuwa na mchango mkubwa dhidi ya Brighton," alisema Arteta kuelekea mchezo wa jana Ijumaa dhidi ya Aston Villa.

"Tangu nimekuwa hapa amecheza mara nyingi na amekuwa muhimu kwenye kikosi chetu."

# Michezo



Jumamosi Oktoba 23, 2021
Nipashe

Haaland anogesha mbio za uhamisho

UKURASA 21




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa (kushoto), akimkabidhi Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, hundi ya mfano ya Sh. milioni 100 ikiwa ni zawadi ya ubingwa wa Ligi Kuu Bara msimu wa 2020/21. Katikati ni Rais wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia na kulia ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah. **PICHA: TFF**

## Yanga yaamsha joto kwa Azam

**Na Mwandishi Wetu**

VINARA wa NBC Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, wanaendelea kujiimarisha kwa ajili ya kuhakikisha wanaondoka na pointi tatu muhimu katika mchezo wao dhidi ya Azam FC unaotarajiwa kuchezwa ifikapo Oktoba 30, mwaka huu.

Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, aliliambia gazeti hili kikosi chake kimeendelea na programu tofauti kwa sababu kila idara inahitaji kupata mbinu ili kufikia malengo.

Nabi alisema anahitaji kuona kila mchezaji anatekeleza vyema majukumu yake katika mchezo huo ambao endapo watashinda, wataendelea kuongoza kwenye msimamo wa ligi hiyo ambayo msimu huu inashirikisha timu 16.

"Tunaijua Azam FC, ni timu bora na ina wachezaji wenye viwango vizuri, wameshinda mechi yao iliyopita, ni wazi wanahitaji kuendelea na ari hiyo, sisi pia tunataka kushinda ili kujiimarisha, tutapambana tu," alisema Nabi.

Aliongeza wanajiandaa kukutana na timu yenye kutumia nguvu kwa sababu watakuwa wametoka kwenye mchezo wa pili wa kimataifa ambao utawasaidia kuwajenga nyota wake.

Katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga yenye pointi tisa iko kileleni wakati Azam FC yenye pointi nne iko katika nafasi ya tisa huku mabingwa watetezi, Simba walio na pointi nne lakini wamecheza mechi moja pungufu wako katika nafasi ya nane.

# SIMBA YANG'ARA TUZO ZA TFF

## Bocco aibuka Mchezaji Bora 2020/21 huku Amina...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Simba, imekabidhiwa hundi ya mfano ya Sh. milioni 100 kama zawadi ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo katika msimu uliopita wa 2020/21 huku wachezaji wake wakitangazwa washindi kwenye sherehe za Tuzo za Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), zilizofanyika jijini Dar es Salaam juzi usiku.

Mbali na Simba kutawala kwenye tuzo hizo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa ambaye alikuwa mgeni rasmi naye alitwaa tuzo ya Rais wa TFF, Wallace Karia kutokana na mchango wake mkubwa kwenye maendeleo ya mchezo huo hapa nchini.

Wakati Simba ikifanya vyema katika upande wa wanaume, watani zao Yanga wenyewe waling'aa zaidi katika soka la wanawake.

John Bocco alitangazwa kuwa mshindi wa tuzo ya Mchezaji Bora akiwashinda Mukoko Tonombe kutoka Yanga na aliyekuwa kiungo wa Wekundu wa Msimbazi, Clatous Chama huku Amina Ally wa Yanga Princess akichukua tuzo hiyo kwa upande wa wanawake.

Bocco alipata tuzo nyingine mbili ikiwamo ya Mfungaji Bora kupitia mabao yake 16 ambayo alifunga lakini vile vile alikuwa katika Kikosi Bora cha msimu huo uliomalizika kilichokuwa na nyota wachezaji 11.

Pia golikipa wa Simba, Aishi Manula, naye alichukua tuzo tatu ambapo alitajwa kama Kipa Bora wa mashindano ya Kombe la FA (ASFC), kwa kuwafunika Faruk Shikhalo (aliyekuwa Yanga sasa KMC) na James Ssetuba wa Biashara United huku tuzo nyingine ni ya Golikipa Bora wa Ligi Kuu Bara na vile vile kuwa kwenye Kikosi Bora cha msimu.

Tuzo ya beki bora wa kushoto iliendа kwa Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', aliyekuwa kiungo wa Simba, Chama aliibuka Kiungo Bora, Simba Queens ikibeba tuzo ya ubingwa wa msimu uliopita sambamba na golikipa wake, Janeth Shija akibeba tuzo ya Golikipa Bora wa ligi hiyo.

Kibwana Shomari wa Yanga alishinda tuzo ya 'Fair Play' huku 'Feitoto' akishinda tuzo ya Mchezaji Bora wa Kombe la FA huku aliyekuwa Kocha Mkuu wa Yanga Princess, Edna Lema, alitajwa kuwa Kocha Bora wa Ligi ya Wanawake wakati Mfungaji Bora wa Kombe la FA alitajwa kuwa ni nyota wa Namungo FC, Reliants Lusajo.

Coastal Union ya Tanga ilishinda tuzo ya timu yenye nidhamu huku nyota wake, Abdul Seleman 'Sopu' akishinda tuzo ya Mchezaji Bora Chipukizi wakati Lambart Sabianka akishinda tuzo ya Goli Bora la msimu uliopita.

Ruvuma Queens ilibeba tuzo ya timu yenye nidhamu katika Ligi Kuu ya Wanawake (SWPL) huku Meneja wa Uwanja wa Nelson Mandela uliopo Sumbawanga, John Zwala, akishinda Tuzo ya Meneja Bora wa Uwanja, Ramadhan Kayoko (Mwamuzi Bora), Frank Komba (Mwamuzi Bora Msaidizi) na Seti Bora ya Waamuzi ilikwenda kwa waamuzi waliochezesha mechi kati ya Simba na Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ambao ni Ahmed Arajiga, Leonard Mkumbo, Hamdani Said na Hellen Mduma.

Amina Kiando alitajwa kuwa Mwamuzi Bora wa Ligi Kuu ya Wanawake, SikudhanI Mkulungwa (Mwamuzi Bora Msaidizi), Bongozozo (Mhamasishaji Bora), Asha Juma (Mchezaji Bora Chipukizi kwa Wanawake) na marehemu Dk. Maneno Tamba akipata Tuzo ya heshima kwa mchango wake katika kuendeleza soka la wanawake huku Rais wa zamani wa TFF, Leodegar Tenga akishinda Tuzo Maalum ya Rais wa TFF, Karia.

Kikosi Bora cha Ligi Kuu ya Wanawake kinaundwa na Janeth Shija, Julieth Singano, Happy Hezron, Violeth Nicholas, Fatuma Issa 'Densa', Amina Bilali, Stumai Abdallah, Oppa Clement, Aisha Masaka na Mawete Mussolo huku kile cha wanaume kinaongozwa na Manula, Kapombe, Zimbwe Jr, Joash Onyango, Job, Mukoko Chama, Feitoto, Bocco, Prince Dube na Luis Miquissone.

**MAJALIWA AWEKA MSISITIZO**

Mbali na kuipongeza TFF kwa kuandaa tuzo hizo, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa alilitaka shirikisho hilo kukaa pamoja na timu zinazopata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ili kufahamu maandalizi yao kwa sababu wanapokwenda kwenye michuano hiyo huiwakilisha Tanzania.

Majaliwa aliitaka TFF na Wizara ya Sanaa, Utamaduni na Michezo, wanakaa pamoja na kuhakikisha safari ya Biashara United kuelekea Libya kurudiana na Al Ahly Tripoli inakamilika huku akiwashukuru wadhamini wote wanaojitokeza kudhamini klabu za soka za hapa nchini.

"Serikali hatuko tayari kuona timu yoyote ambayo inaenda kuwakilisha taifa inashindwa kusafiri kutokana na kukwama fedha za kwenda nchi husika, mfano Biashara United ambao walianza vizuri hatua za awali nje na hapa nyumbani, tuhakikishe timu inakwenda, nina imani kubwa na Biashara United itafanya vizuri katika mchezo huo wa marudiano," alisema Majaliwa.

Kikosi cha Biashara United kilitarajiwa kuondoka nchini jana usiku kwa ndege maalumu ya kukodi ya serikali kwa ajili ya mchezo wao wa marudiano utakaochezwa leo.

Karia aliwataka wadau wote wa soka nchini kuendelea kuwaamini, aliahidi tuzo hizo zitaendelea kuboreshwa huku akiwashukuru wadhamini wote wanaojitokeza kuwekeza katika mchezo huo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >